**RC** Makonda 'amkalia kooni' kamishna ardhi UK. 3



**Samia** kuongoza mkutano nishati safi kupikia



UKURASA 4

**Mzigo** mkubwa wa matibabu kwa magonjwa yasiyoambukiza UKURASA 5



YA KALE NI DHAHABU

UKURASA 13


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Mei 12, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581674

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US






# Majaketi yenye kamera kudhibiti rushwa trafiki

• **Dk.** Mpango ataka wizara kuharakisha mchakato... *uk. 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Askofu Mkuu wa Canterbury na Mkuu wa Kanisa la Kianglikana Duniani, Mhashamu Justin Welby (wa pili kulia) na ujumbe wake, Ikulu jijini Zanzibar jana. Ujumbe huo, uko Zanzibar kwa ajili ya ibada ya maridhiano kutokana na madhila waliyofanyiwa Waafrika wakati wa biashara ya utumwa itakayofanyika leo katika Kanisa la Anglikana Mkunazini. **PICHA: IKULU**

## Askari KINAPA mbaroni tuhuma mauaji ya raia

UKURASA 2



## CCM yambana Lissu kwa madai ya fedha chafu

UKURASA 3

**MICHEZO** MGUNDA: TUMEFUATA POINTI TATU KAGERA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Majaketi ya kamera kudhibiti rushwa trafiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameiagiza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuharakisha mchakato wa matumizi ya majaketi yenye kamera kwa askari wa usalama barabarani, ili kukomesha vitendo vya rushwa ambavyo kwa sehemu, vimekuwa sababu ya ajali.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua kituo kipya cha polisi cha daraja 'A' cha wilaya ya kipolisi Mtumba pamoja na ugawaji wa magari 21.

Alisema wizara hiyo inapaswa kuharakisha mchakato huo wa matumizi ya majaketi ili kusaidia kupunguza rushwa kwa polisi, vitendo ambavyo vimekuwa chanzo cha ajali nyingi nchini.

"Nilikuwa ninazungumza hapa na Waziri (Mhandisi Hamad) Masauni, akanieleza kuwa wako kwenye mchakato wa kuanza matumizi ya majaketi yenye kamera ambayo askari wa usalama barabarani watavaa na yatakuwa yanaonyesha kila kitu na mazungumzo yote yatasikika makao makuu ya trafiki.

"Hivyo basi nikutake Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuharakisha mpango huu ili uanze kufanya kazi na kuondoa tatizo la rushwa kwa askari wetu wa kitengo cha usalama barabarani," alisema Dk. Mpango.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi nchini kujiimarisha kwenye matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ikiwamo matumizi ya kamera za ulinzi (CCTV) ili kudhibiti uhalifu na ajali barabarani.

Pia alilitaka kuongeza matumizi ya roboti pamoja na akili mnemba, lakini pia polisi wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia.

Alisema kutokana na ongezeko la ajali za barabarani, Jeshi la Polisi linapaswa kupitia upya mfumo wa utoaji wa leseni za udereva pamoja na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto, na kuongeza matumizi ya kamera za usalama.

Waziri Masauni alisema kituo hicho kilichozinduliwa ni moja kati ya vituo ambavyo vimejengwa na serikali ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

"Kituo hichi cha kisasa cha daraja A kimejengwa kwa fedha za serikali, lakini pia magari haya 21 uliyogawa leo yatakwenda kufanya kazi katika Wilaya za Kipolisi nchini, na tumeyagawa katika mikoa ambayo ina migogoro ya wakulima na wafugaji," alisema Masauni.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alisema kituo hicho kimejengwa na wataalam wa ndani kwa kutumia mfumo wa Force Account, kimegharimu Sh. milioni 977 na kitahudumia wakazi wa wilaya nane zinazouzunguka mji wa serikali Mtumba.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisikiliza maelezo kuhusu mfumo wa kidijitali wa ufunguaji kesi uliopo katika Kituo kipya cha Polisi Daraja "A" cha Wilaya ya Kipolisi Mtumba, baada ya kukizindua jijini Dodoma jana. Kulia ni Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camillus Wambura. Dk. Mpango pia alikabidhi magari 21 kwa jeshi hilo. **PICHA: OMR**

# Othman asisitiza uchaguzi wa haki

**Na Mwandishi Wetu**

Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema uchaguzi ndiyo mamlaka sahihi ya wananchi na ni njia bora ya kuwapa mamlaka viongozi kusimamia serikali kwa kuweka misingi ya kisera katika kuleta maendeleo.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo juzi wilayani Kahama katika mkutano wa hadhara wakati akikamilisha ziara yake ya kichama ya siku sita katika mikoa ya kanda ya Magharibi ikihusisha Kigoma, Tabora na Shinyanga.

Kutokana na umuhimu huo, alisema ni jukumu la mamlaka zinazohusika na kusimamia uchaguzi kuhakikisha wanafuata misingi iliyowekwa ili kuondoa manung'uniko kutoka kwa wananchi.

Alisema hatua hiyo ndiyo muhimu katika kuleta mageuzi kwa kuwachagua viongozi watakaosimamia serikali kwa kuwajibika kwa uaminifu na uadilifu, hivyo kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii na hatimaye kuwapo maendeleo bora kwa wananchi.

Alisema Shinyanga ni moja ya mikoa muhimu ya Tanzania yenye rasilimali nyingi za kiuchumi kupitia migodi mikubwa ya dhahabu na almasi na pia mzalishaji mkubwa wa mpunga, hivyo una uwezo wa kukusanya fedha nyingi zitokanazo na ushuru, ada na tozo mbalimbali.

Pamoja na kuwapo hali hiyo, alisema bado mkoa huo una ukosefu wa miundombinu na huduma bora mbalimbali kwa wananchi kutokana na kukosekana uwajibikaji bora kwa baadhi ya viongozi wanaopewa dhamana.

Amesema hali hiyo inawafanya wananchi kuendelea kuwa masikini katika utajiri mkubwa wa rasilimali walizo nazo ndani ya nchi kutokana na kukosekana uwajibikaji bora kwa viongozi.

Awali, Othman alitembelea mtaa wa viwanda vya kukoboa mpunga na kuonana na wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda hivyo waliolalamika kwamba eneo hilo licha ya kuwa na faida kubwa kwa serikali, halina mazingira rafiki ya kibiashara kwa kukosa miundombinu muhimu zikiwamo Barabara, hivyo kuongeza gharama katika biashara zao.

Wafanyabiashara hao pia walilalamikia Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kuwa na utitiri wa kodi, tozo na ushuru wa aina mbalimbali na kwamba baadhi ya bidhaa hutozwa mara mbili jambo linalodhoofisha jitihada zao kujikwamua kiuchumi.

Kiongozi Mstaafu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema chama hicho kitaendelea kusemea kero za wananchi kwa kuwa kimejipambanua kwamba ndicho chama cha kutetea maslahi ya Watanzania wote na kuwataka wananchi kukiunga mkono chama kwa kuwapa kura wagombea wao katika uchaguzi wa serikali za vijiji na mitaa utakaofanyika baadaye mwaka huu.

# Askari KINAPA mbaroni tuhuma mauaji ya raia

**Na Maria Mosha,** MOSHI

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amethibitisha kuwapo kwa maandamano yasiyo rasmi ya wanakijiji wa kijiji cha Komela, Kata Marangu Magharibi, kutokana na mauaji ya Octavian Temba (38), anayedaiwa kupigwa risasi na askari wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), Mei 9, mwaka huu.

Babu alisema kulitokea purukushani kati ya askari wa KINAPA pamoja na mwananchi aliyekuwa akikata majani pembezoni mwa eneo la hifadhi na hivyo kupigwa risasi.

"Katika purukushani hizo kulitokea bahati mbaya akapigwa risasi na kupoteza maisha. Jeshi la Polisi limewatia mbaroni askari wawili wa uhifadhi pamoja na wa Jeshi la Akiba (Mgambo) kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

"Ila niwaombe wananchi ikiwa tukio limetokea na tayari wamechukuliwa hatua, siyo vyema kuchukua sheria mkononi. Jana kuna wananchi zaidi 200 walifanya maandamano yasiyo rasmi mpaka kwenye geti la Kinapa, wakafanya vurugu, wameharibu miundombinu," alisema.

Kutokana na tukio hilo, Babu alisema, wananchi wamekata barabara ambayo imejengwa kwa gharama kubwa, wamekata mabomba ya maji na kusababisha baadhi ya wageni kuchukua muda mrefu kutokana na hofu iliyotanda kutokana na maandamana hayo.

Alisema uchunguzi umeonyesha walioandamana siyo vijiji jirani na KINAPA, ni watu kutoka Tarafa ya Vunjo na kulitaka Jeshi la Polisi kuongeza nguvu ya uchunguzi kutokana na ukubwa wa jambo lenyewe.

"Sisi wana Kilimanjaro hatuna tabia ya kufanya vurugu. Hili jambo ni kubwa na halivumiliki, RPC ongezeni nguvu ya uchunguzi haki itendeke, wananchi tunaomba utulivu wa hali ya juu muda huu ambao tunaendelea na uchunguzi," aliomba Babu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alithibitisha kutokea tukio hilo la maandamano yakihusisha wananchi ambao ni wa kijiji alichotoka marehemu baada ya mauaji.

"Upelelezi utafanyika na hatua stahiki zinachukuliwa kulingana na hali ilivyo ni si mihemuko ya kikundi cha watu au mamlaka fulani.

"Tunawashikilia askari wawili wa KINAPA na mgambo mmoja kutokana na mauaji ya kijana huyo, uchunguzi unaendelea na ukikamilika tutawafikisha mahakamani.

"Lakini timu ya madaktari bado haijafanya uchunguzi wa mwili, niwaombe ndugu wa marehemu wafike ili tufanye uchunguzi," alisema Kamanda.

HABARI KITAIFA

## TAKUKURU yaonya uchaguzi wa mitaa

**Na Renatha Msungu** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imewaonya wagombea uchaguzi wa serikali za mitaa kuepuka rushwa ili kuwezesha wananchi kuchagua viongozi sahihi.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, John Joseph, alisema hayo juzi katika semina kwa waandishi wa habari kwa ajili ya kuripoti habari za uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema taasisi hiyo imejipanga kusimamia vyema uchaguzi huo ili kuwa huru na haki ili kupata viongozi bora kwa ajili ya kuwaongoza wananchi.

"Nawaasa viongozi jiepusheni na vitendo vya rushwa. TAKUKURU iko imara kuangalia watoa rushwa na wapokea rushwa," alisema Joseph.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wagombea kuwarubuni wananchi kwa pesa na bidhaa tofauti nak uonye kwamba atakayebainika kufanya hivyo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Kutokana na hilo alisema semina iliyotolewa kwa waandishi wa habari ikawe chachu ya kielimisha jamii kuhusu viashiria vya rushwa mbalimbali pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa.

Alisema taasisi hiyo imejipanga kutoa semina kwa kada mbalimbali kwa lengo la kuona watu wanajua maana ya rushwa, yakiwamo madhara yake kwa mtoa rushwa na mpokeaji.

Kuhusu utoaji elimu kwa jamii, Joseph alisema taasisi hiyo inatoa elimu kwa makundi mbalimbali, yakiwamo ya wanafunzi katika shule za sekondari, msingi na vyuo.

Alisema wanafanya hivyo ili kutaka kuona kila jamii inajua nini maana ya rushwa na wanaelewa madhara ya utoaji na upokeaji rushwa.

Katika hatua nyingine, aliwataka waandishi wa habari kujua mipaka yao katika kuripoti Habari za uchaguzi, huku akiwataka kutokubali kurubuniwa na wagombea.

Alisema wagombea wengi wamekuwa na kasumba ya kutumia pesa ili wapate vyeo jambo ambalo halikubaliki, kutokana na kwamba wanachangia wananchi kuchagua viongozi ambao si sahihi.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dodoma, Katale Mbashiru, aliishkuru TAKUKURU kwa kutoa semina kwa waandishi wa habari jambo ambalo limewasaidia kujua vitu vingi ambavyo walikuwa hawavijui.

Mbashiru alisema elimu waliyoipata itawasaidia katika kuripoti habari za uchaguzi wa serikali za mitaa.

# CCM yambana Lissu madai fedha chafu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Ally Hapi, 'amemtega' Makamu Mwenyekiti Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akimtaka aweke hadharani majina ya wanaohusika na fedha chafu ndani ya chama hicho.

Mei 2, mwaka huu, Lissu akiwa mkoani Iringa, alitoa kauli kuwa ndani ya chama chake, kuna fedha chafu, kauli ambayo ilizua mjadala, huku baadhi wakimkosoa kwa nini asingeongea ndani ya vikao vya chama, na yeye kushangaa kushambuliwa.

Akizungumza na wananchi wa Manispaa ya Singida katika mkutano wa hadhara uliofanyika stendi ya zamani mjini hapa, Hapi alisema Lissu awataje viongozi wenzake ambao anaona wana fedha chafu.

"Lissu anakuja kulalamika kuna fedha chafu katika chama chao zinaenezwa na viongozi, mbona hawataji hao viongozi, atuambie ni nani? Je, ni (John) Mnyika? au (Freeman) Mbowe? au ni nani?," alihoji.

Hapi alimtaka pia, Lissu ataje majina hadharani ya maaskofu na mashehe aliodai kuwa, wamepewa vibali vya sukari kwa kuwa, siasa za uchonganishi zimepitwa na wakati.

**KUPIGA MAJUNGU**

Katika mkutano huo, Hapi alisema Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakitaki kuona watendaji wa serikali wanang'ang'ania maofisi na kupiga majungu, badala yake watoke waende kwenye jamii kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia ufumbuzi.

Alisema CCM ndiyo iliyobeba dhamana ya kuiongoza serikali na hivyo, Mwenyekiti wa CCM Taifa na Katibu Mkuu wa CCM, wametoa maelekezo serikali iendelee kutatua kero za wananchi.

Hapi ambaye yupo katika ziara ya siku nne mkoani Singida alisema pia, CCM haitaki kuona watendaji na watumishi wa umma wenye tabia ya kutoa lugha chafu na kuwakejeli wananchi, hususani kwenye hospitali, vituo vya afya na katika ofisi za umma.

Alisema miradi ya maendeleo ambayo serikali imetoa fedha isimamiwe kikamilifu yeyote atakayedokoa fedha hizo, ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria, na hayo ndiyo maelekezo ya Mwenyekiti wa CCM Taifa ambaye pia, ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

"Niwaombe wananchi 2024 uchaguzi wa vijiji, vitongoji na mitaa usihangaike, tuiunge mkono CCM na 2025 hatuna jambo jingine, mama ndiyo mpango mzima, ana nia njema na nchi yetu, ana uwezo mkubwa wa kusimamia nchi, ni mtu mkweli na mwenye upendo," alisema.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Wazazi wa CCM, Ally Hapi, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara katika Manispaa ya Singida juzi, akiwa katika ziara ya siku nne mkoani humo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Makonda 'amkalia kooni' kamishna ardhi

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, amemjia juu Kamishna Msaidizi wa Ardhi mkoani hapa, Geofrey Mwamsojo, kwa kile alichoeleza kushindwa kutekeleza agizo la Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, la kurejesha ardhi kwa mwananchi.

Makonda alishangazwa na kitendo cha mwananchi mmoja kulalamika kutokupatiwa ardhi hiyo, licha ya Waziri Silaa kutoa maagizo ya kupatiwa haki yake baada ya kupitia taarifa zake na kubaini ni mmiliki halali.

Akisikiliza kero za wananchi juzi jijini hapa katika operesheni maalum ya siku tatu ya kurejesha haki kwa wananchi, Makonda alisema: "Maelekezo ya Waziri yametolewa tangu Machi 16, mwaka huu.

"Huyu mzee wa watu pamoja na uzee wake ni mgonjwa amejikongoja kuja mpaka hapa. Anakuja kufuatilia maelekezo ambayo tayari mmeshapewa. Kwa nini hamtekelezi maagizo ya Waziri Silaa?" alihoji Makonda.

Katika maelezo yake, Kamishna wa Ardhi alithibitisha kuwa tayari wamemwandikia barua aliyefanya dhuluma na tangu Aprili 16, mwaka huu, wanatafuta nyaraka.

"Kiongozi lazima kutakuwa na kitu tunaendelea nacho maana nimekiona hapa. Ni kweli tulikuwa tunamkabidhi," alisema kamishna wa ardhi.

Hata hivyo, pamoja na maelezo hayo, Makonda alihoji kwa nini agizo hilo limechukua muda mrefu.

"Hivi unasikia sauti hizi za watu? Si hawa tu. Hawa wanawakilisha sauti za watu wengi wanaolia kuhusu ardhi. Amekuja Waziri wako, hali ya huyu mzee unaiona. Ukisikia siku amefariki (dunia) akiwa anapigania fedha zake kwa ajili ya matibabu, utajisikiaje? Ungekuwa ni wewe huyu mzee, umekaa hapo, ungechukua hatua gani?,"alihoji.

Katika utetezi wake, kamishna huyo alisema hatua zimeshakamilika wanasubiri kumsajili na kuahidi kwenda kutafuta jalada.

Aidha, Makonda amemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa (RAS), Misaille Musa, kuandika barua rasmi ya kuwataka wakuu wa wilaya kutenga siku tatu za kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

"Tukifika katika ziara wilayani kwako, kwa mfano tukiwa Karatu, mkuu wa wilaya atuambie huyu tulimsikiliza na kutatua kero yake kwa namna fulani na tumekwama eneo hili. Mkuu wa Mkoa tusaidie hapa tumekwama'," alisema.

Makonda alibainisha kwamba heshima ya jambo hilo iko maeneo ya mijini lakini wakiingia wilayani ni kama vile hakuna watu wa mipango miji, hivyo akawataka watendaji wote kuhakikisha wanasimamia ipasavyo sekta ya ardhi.

"Viwanja vinavyochangamkiwa ni vile vyenye fedha, vile vyenye hali ya chini ndiyo hamwonekani. Mnajisahau hawa wa hali ya chini ndiyo wanatupigia kura ili tuendelee kuwapo," alisisitiza.

Makonda alisema Mei 20, mwaka huu, ataanza ziara katika wilaya zote za mkoani hapa ili kuhakikisha kila mwananchi anapatiwa haki yake, na kuwataka watendaji watatua kero za wananchi.

Alisema wananchi wengi wanaumizwa kwa kuwa, hawajui sheria na kueleza kuwa, ni wajibu kwa viongozi kuwasaidia ili wapate haki zao.

HABARI KITAIFA

## Biteko ataka Msalaba Mwekundu kushiriki kwenye uokozi majanga

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amekiagiza Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) kushiriki katika majanga mbalimbali na sherehe za kitaifa, ili kusaidia kutoa huduma ya kwanza pale watu wanapopata matatizo.

Dk. Biteko alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye maadhimisho ya miaka 62 ya chama hicho.

Alisema Chama cha Msalaba Mwekundu ni chama muhimu kwa jamii, hivyo wanapaswa kushiriki katika makongamano na mikusanyiko mbalimbali ili kutoa huduma kwa wananchi.

Biteko alisema chama hicho kinapaswa kuwa mstari wa mbele katika utoaji wa huduma ya kwanza katika jamii hususan kunapokuwa na matukio mbalimbali au sherehe.

Kadhalika alisema kinapaswa kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufanya kazi zao kila sehemu ambako wanahitajika ili kuisaidia jamii.

"Mnaazimisha miaka 62 ya chama chenu, hivyo fanyeni kazi kwa bidii ya kuhudumia jamii ili muweze kupanua wigo wa chama chenu," aliagiza.

Mbali na hilo, Dk. Biteko aliwapongeza Red Cross kutokana na utendaji kazi wanaofanya na kuwataka waongeze bidii katika utoaji wa huduma zao za kila siku.

"Kitengo hichi ni cha muhimu sana kwa jamii, hivyo mnapaswa kuchapa kazi kwa bidii ili mzidi kutambulika na jamii,"aliagiza.

Rais wa chama hicho, David Kihenzile, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Uchukuzi, alisema wamekuwa wakipata takwimu nyingi za wagonjwa ambao wanapata msaada kutoka Red Cross na kuokoa maisha ya wanadamu.

Alisema watazingatia kile walichoagizwa na Naibu Waziri Mkuu ,na kuahidi kwenda kufanyia kazi ili waweze kusonga mbele katika utendaji kazi wao.

"Tunajua umuhimu wetu ndiyo maana serikali inatambua mchango wetu, tunaahidi tutazidi kuboresha huduma zetu kwa jamii," alisema.

Alisema wameadhimisha miaka 62 ya chama na watazidi kuboresha huduma zao kwa jamii ili wazidi kuonekana mbele kwa wananchi.

Alisema lengo lao ni kuona jamii inawatambua kutokana na kazi zao za kila siku wanazofanya kwa jamii za utoaji huduma za kiafya.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ziara ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan nchini Ufaransa, kwa ajili ya kushiriki katika mkutano wa wakuu wa Nchi za Afrika wa mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia kuongoza mkutano nishati safi ya kupikia

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajia kufanya ziara ya siku nne kuanzia leo Paris, nchini Ufaransa, kushiriki mkutano wa wakuu wa nchi kuhusu nishati safi ya kupikia kwa Afrika.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu ziara hiyo, alisema itaanza leo hadi Mei 15, mwaka huu, na kwamba Rais atashiriki mkutano huo utakaofanyika keshokutwa.

"Ushiriki wa Mheshimiwa Rais kwenye mkutano huo umetokana na ombi la Dk. Fatih Birol, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kimataifa ya Nishati ambapo Mheshimiwa Rais aliliridhia kuwa Mwenyekiti Mwenza wa mkutano huu. "Wenyeviti wenza wengine ni yeye mwenyewe Dk. Fatih; Jonas Gahr Store, Waziri Mkuu wa Norway; na Dk. Akinwumi Adesina, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)," alisema.

Makamba alisema kaulimbiu ya mkutano huo inasema 'Nishati Safi ya Kupikia kwa Afrika'. Lengo la mkutano huo ni; kulifanya suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia kuwa la kipaumbele katika ajenda ya kimataifa," alisema.

Malengo mengine aliyataja kuwa kuainisha hatua madhubuti za kisera zitakazoharakisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; na kutoa fursa ya washiriki kutoa ahadi za kifedha, sera na ubia ili kufikia azma ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Tanzania, inashiriki katika mkutano huu wakati Mheshimiwa Rais akiwa kinara wa ajenda hii ya nishati ya kupikia kutoka Afrika.

"Mtakumbuka kuwa, wakati wa Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu, Novemba 30, mpaka 12, Desemba 2023.

"Mheshimiwa Rais alizindua Programu ya Nishati Safi ya Kupikia ya Kusaidia Wanawake Barani Afrika (African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP) na hivyo, kumfanya kuwa championi wa agenda ya nishati safi ya kupikia barani Afrika," alisema Makamba.

Waziri huyo alitaja matarajio ya ushiriki wa Tanzania katika mkutano huo ni, Rais Samia kuendelea kuibeba vyema ajenda hiyo kwa niaba ya Wakuu wa Nchi za Afrika.

"Lakini ushiriki wetu pia ni fursa ya kuonyesha hatua kubwa ambazo tumepiga kama nchi katika kushajiisha ajenda hii ya nishati safi ya kupikia," alisisitiza Makamba.

Alisema mialiko imetumwa kwa Wakuu wa Nchi za Afrika na Viongozi wa Taasisi na kampuni za kimataifa zinazohusika na niishati safi ya kupikia.

Alisema watu wengine mashuhuri wanaotarajia kushiriki kwenye mkutano huu ni, Antonio Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (ujumbe wa video); Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO); Michelle Bachelet, Rais Mstaafu wa Chile na Kamishna Mkuu Mstaafu wa Haki za Binadamu (2018 – 2022).

Wengine ni Mary Robinson, Rais Mstaafu wa Ireland na Kamishna Mkuu Mstaafu wa Haki za Binadamu (1997 -2002); Dk. Sultan Al Jaber, Rais wa Mkutano wa 28 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP28); Mukhtar Babayev, Rais ajaye wa COP29 na Waziri wa Ikolojia na Maliasili wa Azerbaijan na Mo lbrahim, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa taasisi ya Mo Ibrahim na wengineo.

"Hadi sasa zaidi ya washiriki 900 walikuwa wamejiandikisha kushiriki kwenye mkutano huo, wakiwamo wawakilishi wa serikali; wadau wa maendeleo; taasisi za kifedha; mashirika yasiyo ya kiserikali; sekta binafsi; wanataaluma; asasi za kiraia; na wawekezaji," alisema.

Kuhusu mkutano huo, Makamba alisema ratiba ya mkutano wa kilele imegawanyika katika sehemu tatu: ufunguzi uliopewa dhima ya Making 2024 a Turning Point for Clean Cooking.

Alisema Rais Samia atashiriki kwenye ufunguzi ambapo yeye pamoja na wenyeviti wenza watapata fursa ya kutoa hotuba ya ufunguzi, na baada ya hotuba, viongozi wengine mashuhuri, akiwamo Julius Maada Bio, Rais wa Sierra Leone watapewa wasaa wa kutoa hotuba muhimu.

Alisema hotuba hizo zitafuatiwa na mjadala wa jopo wenye dhima isemayo Elevating Clean Cooking on the Global Energy, Health, Development, Gender, Environment and Climate Agenda, utakaoendeshwa na Michelle Bachelet, Rais Mstaafu wa Chile.

Alisema sehemu hiyo ya ufunguzi itahitimishwa kwa ujumbe mfupi wa video wa Antonio Guterres, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na pia, kutakuwapo na mijadala mbalimbali

Alisema sambamba na mkutano wa wakuu wa nchi, kutakuwa na matukio ya pembezoni ambayo yanalenga kuonesha, kutangaza na kuvutia fursa za uwekezaji katika masuala ya nishati safi ya kupikia.

Makamba alisema Rais Samia pia, atapata fursa ya kufanya mazungumzo ya uwili na Emmanuel Macron, Rais wa Ufaransa, ambayo yatafanyika Jumanne ijayo katika Ikulu ya Elysee, Paris, Ufaransa.

Kadhalika alisema Rais Samia atakutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa kiserikali na taasisi za sekta binafsi pembezoni mwa mkutano huo.

Makamba alisema utatoka na tamko la pamoja litakaloonesha utashi thabiti wa kisiasa katika kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia ambalo litasainiwa na viongozi watakaoshiriki kwa niaba ya serikali na taasisi zao.

Kadhalika alisema kutakuwapo na muhtasari wa mwenyekiti utakaotolewa na Dk. Fatih kwa niaba ya wenyeviti wenza wa mkutano huo, ambao utabainisha masuala muhimu yaliyoibuliwa katika mkutano zikiwamo ahadi za hatua madhubuti za kukuza ajenda ya nishati safi ya kupikia barani Afrika na duniani kwa ujumla.

# Wizara yabanwa ushiriki wazawa katika ujenzi

**Na Romana Mallya**

NAIBU Spika Mussa Azzan Zungu (Mb), ameitaka Wizara ya Ujenzi kukamilisha maboresho yaliyotolewa na wabunge kuhusu mkakati wa kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi, ili Bunge kuja na mkakati wa pamoja kati yake na serikali.

Zungu aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati wa semina iliyoandaliwa na wizara hiyo kwa wabunge ili kuwajengea uelewa wa mikakati ya ushiriki wa makandarasi na washauri elekezi wazawa kwenye miradi.

"Hauwezi kufanikiwa bila kufanya makosa, na kama utaogopa kufanya makosa hutaweza kufanikiwa, makosa mengi mmefanya na mmeainisha sasa mnataka kwenda kuyafanyia kazi na kuleta maendeleo ya taifa letu na kwa hili nawapongeza serikali", alisema.

Zungu alisema kutokana na changamoto ya fedha za serikali kwenda nje kwa miradi inayotekelezwa na makandarasi kutoka nje ya nchi, serikali imeona umuhimu wa kuweka mikakati madhubuti wa kuweza kuwanufaisha makandarasi na washauri elekezi wazawa kwa kuwashirikisha kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Aidha, Naibu Spika alitoa rai kwa taasisi za kifedha kuangalia namna ya kupunguza riba kwa kuwa, zinazosababisha kurudisha nyuma makandarasi na kampuni za makandarasi ambao huchukua mikopo kwenye taasisi hizo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Selemani Kakoso (Mb), ameitaka wizara hiyo kuhakikisha inasimamia wazawa kutekeleza miradi inayotekelezwa kwa ubora na kwa wakati ili iwe mifano katika maeneo mbalimbali.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema tathmini iliyofanyika katika kipindi cha miaka 10 kuanzia Mwaka 2013 hadi 2023, inaonyesha miradi yenye thamani ya Sh. trilioni 61.64 ilisajiliwa na kutekelezwa nchini ambapo kati ya hiyo wazawa wametekeleza asilimia 38.5 na asilimia 40 ilitekelezwa na makandarasi wa nje ambao kwa ujumla wake hawazidi 500.

Alisema inaonesha kuwa miradi yenye thamani kubwa mingi imetekelezwa na makandarasi wa nje.

Ameeleza faida za mkakati huo kuwa utasaidia kuongeza wigo wa ajira katika sekta ya ujenzi, kujenga, kukuza ujuzi na uzoefu na hivyo, kutekeleza miradi mikubwa pamoja na kuokoa fedha za kigeni na kuhakikisha fedha hizo zinabaki nchini.

"Mkakati huu unakwenda kujibu changamoto ambazo zimekuwa zikiwasilishwa na wazawa serikalini na ni muda sahihi wa wizara kushirikiana na wizara nyingine kuhakikisha mpango mkakati huu unafanikiwa," alisema Bashungwa.

Mkakati wa kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi una lengo la kuwajengea uwezo hatua kwa hatua makandarasi, washauri elekezi na watalaam wazawa, ili waweze kutekeleza miradi mikubwa ya ndani na hatimaye kushindana kimataifa.



Waendesha pikipiki na bajaji wakiwa wamekwama katika barabara ya Uhuru, eneo la Karume, jijini Dar es Salaam jana, kutokana na msongamano mkubwa wa magari. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Matibabu magonjwa yasioambukiza mzigo

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hivi sasa fedha nyingi zinatumika kutibu magonjwa yasiyoambukiza, iwe ni kwa serikali au mtu mmoja mmoja na kwamba yanapoteza nguvu kazi ya taifa.

Kutokana na hilo, Majaliwa amehamasisha michezo huku akieleza ni zaidi ya afya na burudani, ni fursa ya ajira na pia hupunguza magonjwa mwilini.

Akizungumza jana na viongozi, wananchi na washiriki waliohudhuria hafla ya kufunga hafla ya TULIA MARATHON iliyofanyika katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, Mbeya, Majaliwa alisema kwa mujibu wa Wizara ya Afya, michezo inawezesha watu kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

"Kama mnavyofahamu, michezo ni zaidi ya afya na burudani, lakini leo (jana) tumethibitisha kuwa baada ya mbio hizi, sote tumefurahi na miili yetu imeimarika.

"Taarifa za wizara zinasema nchi yetu inakabiliwa na changamoto ya ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu, kisukari, kiharusi na maumivu ya viungo kama magoti na mgongo kwa hiyo, tujenge tabia ya kufanya mazoezi, " alihamasisha.

Majaliwa pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuboresha michezo na hivyo kuongeza hamasa ya kitaifa ya kupenda michezo.

Alisema alianzisha mpango wa Goli la Mama, Changizo la Kitaifa kwa ajili ya timu za kitaifa ikienda sambamba na michezo ijayo ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027).

Majaliwa aliagiza Wizara ya Maliasili na Utalii izitumie mbio za Tulia Marathon kutangaza utalii wa mkoa wa Mbeya na mikoa ya jirani.

"Mkoa huu una vivutio vingi na mikoa ya jirani inavyo vivutio mbalimbali. Tumieni mbio hizi kuwa fursa ya kutangaza utalii. TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) wekeni banda hapa, onyesheni kuna vivutio gani kwenye mkoa huu na mikoa ya jirani," aliagiza.

Pia aliwataka wafanyabiashara na wakulima wa mkoa huo na mikoa jirani watumie mbio hizo kama jukwaa la kutangaza biashara zao na kupata masoko.

Kadhalika aliitaka taasisi ta Tulia Trust ione umuhimu wa kupanua mbio hizo ili kujumuisha pia, washiriki kutoka nchi nyingi zaidi za jirani.

"Ninatambua sasa hivi kuna washiriki kutoka Kenya na Uganda, ni vema sasa uongozi wa Tulia Trust, ukaona namna ya kupanua mialiko hadi nchi jirani za Malawi, Zambia, Congo na Msumbiji ili zipande hadhi na kuwa za kimataifa," alisema.

Spika wa Bunge na Rais wa Mabunge ya Dunia (IPU), Dk. Tulia Ackson, ambaye pia ni mwasisi wa mbio hizo, alisema taasisi hiyo ilikuwa ikijielekeza kutatua changamoto za miundombinu ya elimu na afya, lakini sasa inalenga kuja na kitu kipya kwa sababu vyote vinafanywa na serikali.

"Tunahitaji kupata ekari 15 za kujenga kituo cha kukuza vipaji vya vijana wanaopenda riadha. Tunatarajia kuanza ujenzi huo mwaka huu, kituo hicho kikikamilika kitakuwa kinatumiwa na watu kutoka nchi nzima na nje ya nchi," alisema.

Alisema miaka ya nyuma walikuwa wakinunua madawati, madaftari ya wanafunzi na kujenga madarasa, mabweni, pamoja na kusaidia kwenye huduma za afya, lakini kwa sasa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya miundombinu hiyo.

Dk. Joyce Komba kutoka Hospitali ya Mkoa wa Rufani ya Mbeya alisisitiza umuhimu wa wananchi kufanya mazoezi kila mara ili kuboresha afya na kupunguza changamoto ya magonjwa yasiyoambukiza.

Waziri Mkuu alimkabidhi Bibi Maligo Diamond nyumba ya vyumba vitatu ambayo imejengwa na taasisi ya Tulia Trust ili kumsaidia kutoka kwenye changamoto ya maisha duni na kumwezesha aishi maisha bora yeye na familia yake.

Kupitia mbio hizo, Majaliwa alikabidhi medali na zawadi za fedha taslimu kwa washindi wa kwanza hadi wa tatu wa mbio za kilometa 10, kilometa 21 na kilometa 42.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria ifanyiwe mabadiliko ili kuibana mifuko ya jamii

**KWA** miaka mingi, kumekuwa na kilio cha wastaafu kucheleweshewa mafao yao katika mifuko ya jamii ama kutokana na kumbukumbu zao kutokuwa sahihi au baadhi ya makato kutokupelekwa na waajiri kwa wakati.

Matokeo ya kuwapo kwa adha hiyo ni wastaafu wengi kushindwa kupata fedha zao kwa wakati baada ya kustaafu, hivyo kuishi maisha magumu na ya shida ambayo wakati mwingine huwasababisha kupata maradhi kama ya moyo, shinikizo la damu, sonona na msongo wa mawazo. Licha ya kupata maradhi hayo kutokana na kukosa stahiki zao walizozitolea jasho kwa miaka 30 na zaidi, baadhi hupoteza maisha. Jambo lingine ambalo limekuwa likisababisha wastaafu hao kutokupata mafao yao kwa wakati ni baadhi ya maofisa wa mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ndiyo husimamia fedha za wastaafu hao walizokuwa wakikatwa kila mwezi kwa muda wao wote wa utumishi, kuendekeza rushwa. Kuna msemo ambao hutumiwa na baadhi ya maofisa hao kwamba mkono mtupu haulambwi, hivyo ili kupata mafao lazima mstaafu aachie sehemu ya fedha hizo. Ukishindwa kutoa kubali kupata maumivu usiyotarajia.

Kuwapo kwa hali hiyo kumesababisha baadhi ya watu kuwa katika majuto na hata wale walioko katika utumishi wanaona hakuna faida ya kujituma na matokeo yake hujiingiza katika vitendo vya udokozi na ubadhirifu wa fedha. Hiyo inatokana na hali halisi iliyopo wanapowaona wastaafu wakitaabika kufuatilia mafao yao kwenye ofisi za mifuko ya jamii na kuambulia patupu.

Kwa mantiki hiyo, wafanyakazi hao wanaona hakuna haja ya kuwa waaminifu na kujituma katika kazi kutokana na mateso wanayoyaona kwa waliowatangulia ambao licha ya kutoa jasho jingi katika utumishi na kwa uaminifu, wanaishia kuwa ombaomba na wenye taabu tupu.

Hali hiyo, baada ya kukithiri na kuwa kero na maumivu kwa wastaafu, imesababisha bunge kuingilia kati na kutaka mifuko hiyo ya jamii ibanwe kwa kuchelewesha mafao ya wastaafu. Katika kutaka mifuko hiyo ibanwe, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, juzi alitoa ushauri kwa serikali kuandaa mpango wa kubadili sheria ili kuweka riba kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii itakayochelewesha mafao.


Hatua hiyo ilitokana na majibu ya serikali kuhusu adha wanazopata wastaafu baada ya Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, kusema wako wastaafu waliokuwa kwenye mifuko ya zamani kabla ya kuunganishwa na kuanzishwa Mfumo wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na ule wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ambao wanadai mafao yao kwa muda mrefu lakini mpaka sasa hawajalipwa.

Pamoja na majibu ya serikali, Spika Tulia alisema kuna watumishi wanaostaafu kwa sasa wanasotea mafao kuanzia miezi sita hadi mwaka, hivyo kusema ili kuhakikisha jambo hilo linakomeshwa, serikali ifanye mabadiliko ya sheria katika mifuko ili mafao ya wastaafu yanapocheleweshwa, kuwapo na riba. Kwa mantiki hiyo, kuwe na riba ya asilimia fulani ya mafao ya mstaafu ili mifuko hiyo ione uchungu wa kulipa ziada pale inaposhindwa kuwalipa wastaafu hao kwa wakati. Ni ukweli kwamba kilio cha ucheleweshaji mafao, licha ya kwamba watumishi hao huambulia kiduchu licha ya kufanya kazi kwa muda mrefu, kimekuwa kero kubwa sawa na ugonjwa usio na tiba. Iwapo sheria hiyo ikibadilishwa na mifuko ikatozwa riba, itajifunza somo zuri na hatimaye kuwajibika ipasavyo.

Licha ya serikali kusema kuwa serikali ilishaboresha mfumo wa malipo ya pensheni na kwamba taarifa za wastaafu zinaandaliwa miezi sita kabla ya kustaafu na ndani ya siku 60, mhusika analipwa mafao yake. Majibu hayo ya serikali ni ya kinadharia zaidi kuliko uhalisia kwa sababu wastaafu wengi wanazungushwa na matokeo yake baadhi hukata tamaa.

Kuna msemo kwamba sheria ni msumeno na kwamba katika sheria ya hifadhi ya jamii, mwajiri anayechelewesha inamtaka alipe riba. Sasa iweje sheria hiyo inakata upande mmoja badala ya pande zote mbili?

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wadau wa elimu wasaidie kumaliza vikwazo

**BAADHI** ya shule za msingi na sekondari nchini, zina uhaba wa matundu ya vyoo kitendo kinachosababisha usumbufu kwa wanafunzi wanapohitaji kupata huduma hiyo muhimu.

Kwa mfano, Februari, mwaka huu, vyombo vya habari viliripoti kuwapo kwa uhaba wa matundu vya vyoo katika Shule ya Msingi Kahama, iliyoko Manispaa ya Ilemela jijini Mwanza.

Inaelezwa kuwa shule hiyo ina wanafunzi 1,963 na matundu 15 tu ya vyoo, na kwamba uhaba huo unasababisha wanafunzi 130 kutumia tundu moja la choo kwa siku.

Katika maeneo mengine ya nchi, inaelezwa kuwa baadhi ya shule zina uhaba wa vyoo unaosababisha wanafunzi kujisaidia vichakani au katika vyoo vya nyumba za jirani na shule.

Kwa ujumla ni kwamba shule nyingi zina tatizo, ambalo wakati mwingine ni hatari kwa afya za wanafunzi na pia usalama wao, hasa vyoo ambavyo vina nyufa.

Katika mazingira hayo ya uhaba wa vyoo, baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakiripotiwa kujisaidia choo kimoja na walimu wao, kitendo ambacho kimsingi si heshima.

Ninadhani hali hiyo inaweza kurudisha nyuma juhudi za walimu katika kutoa taaluma, kwani ni vigumu kwa mtoto kujifunza katika mazingira haya.

Ingekuwa ni vyema sasa kuwapo kwa kampeni maalum za kuhakikisha kila shule inakuwa na matundu ya kutosha ili kuondolea adha hii wanafunzi na walimu.

Tunaambiwa kuwa kampeni ya 'nyumba ni choo' imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhamasisha wananchi kuwa na vyoo vya kisasa, ninadhani kampeni hiyo ingehamia shuleni pia.

Ikumbukwe kuwa tatizo la uhaba wa vyoo sasa limeota mizizi katika shule za msingi na sekondari, ni wazi hazina vyoo vinavyokidhi mahitaji ya wanafunzi.

Hivyo, ni vyema kampeni hiyo ingetua shuleni ili kamati na bodi za shule zihamasike na kuona umuhimu wa shule kuwa na vyoo vya kutosha na tena bora.

Shule hizo ni za umma, hivyo umma hauna budi kuzihudumia kadri inavyowezekana kuanzia chakula cha wanafunzi na hata ujenzi wa miundombinu, ikiwamo ujenzi wa vyoo na hata madarasa.

Kamati na bodi ndizo zenye kupanga mipango ya kuboresha shule kwa kushirikisha wananchi ili waweze kuzihudumia badala ya kujiweka pembeni na kudhani hawahusiki.

Sidhani kama ni kosa wananchi kuchimba mashimo ya vyoo, kufyatua matofali na kujenga na kwa ajili ya watoto wao. Suala la msingi hapa, ni kuimarisha mfumo wa ushirikishaji wa wananchi kwa mambo ambayo yanawahusu, ili nao wawe na mchango.

Binafsi ninaamini kwamba ujenzi wa vyoo vya shule umo ndani ya uwezo wa umma si wa kutafuta au kusubiri wafadhili. Jambo la muhimu ni ushirikishaji. Umma au jamii inapaswa kujishughulisha na tatizo hilo la wanafunzi kukosa vyoo, kwa kupitia kamati na bodi za shule, huku serikali ikitia msukumo.

Kamati na bodi za shule zikifanya sehemu yake ya kushirikisha na kuhamasisha wananchi huku serikali nayo ikitia msukumo, tatizo la uhaba wa vyoo au shule kuwa na vyoo vibovu inaweza kuwa ni historia.

Ikumbukwe kuwa majukumu ya kamati na bodi za shule ni pamoja na kuandaa mipango wa maendeleo ya shule, kuhakikisha shule inakuwa na miundombinu na vifaa kamili na bora.

Vilevile, ni kutafuta vyanzo vya fedha kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya shule, hivyo, ukubwa wa tatizo la vyoo katika shule za msingi na sekondari linaweza kuisha iwapo kamati na bodi zitawajibika vizuri.

Hapa kinachohitajika ni ubunifu na weledi wa kutatua kero za uhaba zinazozikabili shule badala ya kusubiri fedha kutoka serikalini, huku wananchi wapo ambao ndio wenye shule.

Kamati na bodi zinaweza kubuni vyanzo vingine vya mapato ili kuboresha miundombinu ya shule, lakini pia wakati mwingine inawezekana kutatua tatizo la kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira husika kama miti, mchanga na mawe na rasilimali watu kumaliza tatizo hilo sugu.

Aidha, kamati na bodi zinaweza kutoa elimu kwa wanajamii ili zitambue shule za umma ni mali yao, hivyo wazihudumie kadri inavyohitajika badala ya kuachia serikali jukumu hilo.

**SAFU**

**FIKRA MBADALA**

# Pongezi serikali, TEF kuhamasisha matumizi ya gesi



**Pascal Mayalla**

KWA nini vyombo vya habari havishirikishwi kikamilifu katika programu muhimu za mipango mkakati mbalimbali hapa lakini wakati wa utekelezaji, inakumbukwa na kuitwa waandishi kwa kuwasomba mzobe mzobe na kuwalipa posho kiduchu, wakati wenyewe mmelipana vizuri?

Nijuavyo, kila program lazima ina kitu kinachoitwa mkakati wa mawasiliano (communication strategy). Kila wizara, idara, taasisi na kila programu, lazima iwe na huo na bajeti yake ya kueleweka.

Hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, alizindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 jijini Dar es Salaam. Katika uzinduzi huo, Rais Samia alisema: "Serikali tunalo jukumu la kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu nishati safi ya kupikia na kutunga sera nzuri na wezeshi ili kufikia malengo ya mkakati huu. Katika hili wenzetu wa Wizara ya Nishati watatuongoza kuhakikisha nishati safi ya kupikia inapatikana kwa uhakika na kwa bei inayohimilika kwa wananchi."

Nilipopitia kabrasha la mpango huo, sikufanikiwa kuona mkakati wa mawasiliano na hao watakaofanya huo uelewa kwa wananchi, kama si sisi vyombo vya habari ni nani? Kwa nini vyombo vysa habari vinapuuzwa katika maadalizi na matokeo yake vinaitwa tu wakati wa tukio lenyewe kama lile la uzinduzi?

Angalau Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), limeonyesha mfano kwa kuwaita na kuwakutanisha wahariri kutoka katika maeneo mbalimbali nchini waliojumuika jijini Dodoma kuhudhuria Mkutano Mkuu wa 13 wa Kitaaluma wa Jukwaa la Wahariri, uliofanyika Aprili 29 hadi 30, mwaka huu. Mkutano huo ulibeba kaulimbiu isemayo 'Uandishi wa Habari Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Kulinda Misitu'.

Mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ambaye aliipongeza TEF kwa kusema: "Kama kuna jambo zuri mnalolifanya TEF ni kukutana kila mwaka na kujitathmini. Mkutano huu wa kitaaluma unawapa fursa ya kupitia utendaji wenu."

Dk. Biteko aliwaasa waharir kuutumia mkutano huo kuona kama taaluma iko sawa sawa huku akisema: "Mmepata wavamizi wanaoitwa mMakanjanja'. Kuna watu wanajipachika uandishi wa habari huko, wanapiga simu kwa watu mbalimbali na kudai fedha kwa vitisho kuwa wasipopewa watawalipua. Hili nalo mliangalie."

Kuhusu matumizi ya gesi, Biteko alisema: "Ziko faida nyingi unapotumia gesi ambazo kati yake kubwa ni ulinzi wa misitu, hivyo kuliepusha taifa na dunia na hatari ya jangwa. Tunapokata misitu, tunaharibu ardhi. Nyote mnafahamu kuwa dunia imemchagua Rais Samia (Suluhu Hassan) kuwa Kinara wa uhamasishaji matumizi ya nishati safi ya kupikia, ambayo ni gesi kwa Bara la Afrika.

"Kwa mabara mengine kama Ulaya, Amerika ya Kusini na Kaskazini na Asia, kwa muda mrefu wamekuwa wakitumia nishati ya gesi kwa ajili ya kupikia majumbani. Kwa mabara haya, kukata mti kwa ajili ya kuni au mkaa inachukuliwa kuwa ni uhalifu usiokubalika.

"Wenzetu wanatumia gesi kwa ajili ya kupikia, mfumo wa joto katika nyumba zao katika kipindi cha majira ya baridi, na kama Mwenyekiti alivyosema, gesi inatumika sasa kuendeshea magari. Sisi kama Wizara ya Nishati tumeandaa mpango kabambe wa kuhamasisha matumizi ya gesi nchini."

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, aliipongeza serikali imeleta nafuu kubwa katika uhuru wa kutoa mawazo, uhuru wa kukusanyika, kuabudu, kukusanya, kuchakata na kuchapisha taarifa bila kujali mipaka ya nchi.

"Tangu 2016 hadi leo, tumekuwa tukisubiri serikali ianzishe taasisi zinazoanzishwa na sheria hiyo ambazo ni pamoja na Bodi ya Ithibati, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Wanahabari kwani tumevisubiri kitambo vyombo hivi, ambavyo vikianzishwa sisi wanahabari tutapumua," alisema Balile.

Kauli mbiu hii "Uandishi wa Habari Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Kulinda Misitu." imebeba ujumbe unaozingatia kwamba Rais Samia, Novemba, mwaka jana, alichaguliwa kuwa kinara (champion) wa Ajenda ya Nishati Safi na Salama ya Kupikia kwa Wanawake wa Afrika katika mkutano wa COP28 uliofanyika Dubai.

Kwa kutambua hilo, TEF iliona ni bora vyombo vya habari navyo vishiriki kuunga mkono nia hiyo njema ya Rais Samia na hasa kwa kutambua kwamba suala muhimu.

Balile alisema wakati wakitafakari nafasi ya kaulimbiu hiyo, walibaini kuwapo kwa dalili za rasilimali ya gesi kutotumika ipasavyo kutatua changamoto hasa katika sekta ya nishati, kwa maana ya upatikanaji wa umeme nchini na kutumiwa kama nishati safi ya kupikia kwa akina mama, licha ya kujengwa bomba la kusafirisha rasilimali hiyo kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam, ambalo ujenzi wake uligharimu mabilioni ya shilingi za Kitanzania.

Balile alisema: "Bomba hili kwa taarifa tulizo nazo linatumika kwa kiwango cha chini kwani miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi pale Kenyerezi, Dar es Salaam haijafanya kazi kwa idadi ya megawati zilizokusudiwa. Tuliahidiwa Kinyerezi I, II, III na IV, lakini taarifa tulizo nazo, Kinyerezi III na IV hazijafanya kazi kwa kiwango kilichokusudiwa.

"Sisi Wahariri, tunatamani kuona mchango wa rasilimali gesi katika uchumi wa nchi yetu na watu wake, na zaidi kusaidia taifa kuondokana na changamoto ya akina mama wenye macho mekundu kutokana na moshi wa kuni kudhaniwa kuwa ni wachawi na kuuawa katika baadhi ya mikoa hapa nchini.

Kwa upande wangu, naendelelea kusisitiza, vyombo vya habari ni wadau muhimu, hivyo ni lazima vshirikishwe katika mipango yote kwa kuwa na mkakati wa mawasiliano.

**Paskali**
**0754 270403**

# Mtaalamu aanika uzalishaji mdogo dawa

**Na Joseph Mwendapole**

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Patrokil Kanje. amesema soko la dawa la Tanzania ni miongoni mwa masoko kubwa Kusini mwa Jangwa la Sahara lakini bado halijatumika kikamilifu.

Dk. Kanje alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akiwasilisha matokeo yake ya utafiti kuhusu mnyororo wa thamani wa sekta za nguo, dawa na usindikaji wa vyakula nchini.

Aliwasilisha mada hiyo kwa wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) katika mkutano wa uchambuzi wa mnyororo wa thamani wa sekta za kimkakati za viwanda vya nguo, dawa na usindikaji wa chakula nchini Tanzania.

Dk. Kanje alisema kuna viwanda 42 tu vya kutengeneza bidhaa za binadamu na 18 kati ya hivyo, vinajishughulisha na utengenezaji wa bidhaa za dawa na vifaa vya matibabu vikiwamo 24.

Alisema uwezo wa viwanda ni mdogo katika bidhaa mbalimbali na kimsingi huzalisha dawa za aina moja pekee na kwamba kutokana na hali hiyo, Tanzania inabaki kuwa mwagizaji wa jumla wa bidhaa zake za dawa.

Alisema ushahidi kutoka kanzidata ya Umoja wa Mataifa ya COMTRADE kuhusu biashara ya kimataifa, unaonyesha kuwa mwaka 2021 zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa za dawa zenye thamani ya dola milioni 458.7 ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

Dk. Kanje alisema uwezo wa ndani wa kuzalisha dawa nchini umepungua kutoka asilimia 33 mwaka 2009 hadi kati ya asilimia 10 na 20 mwaka 2022.

"Hii ina maana kwamba wakati soko limekuwa likikua kwa wastani wa asilimia tisa kwa mwaka, thamani ya bidhaa za ndani sokoni imekuwa ikishuka na kufikia kati ya asilimia 10 na 20," alisema.

Dk Kanje alisema licha ya nia njema ya uingiliaji kati wa sera na juhudi kubwa za serikali kuziboresha, mfumo uliopo wa udhibiti na utendaji wake una sifa ya udhibiti mkubwa ambao umefikia gharama kubwa ya anzisha biashara.

"Gharama kubwa ya kusajili biashara inaathiri ushindani wa ndani na kimataifa wa biashara hizi na kusababisha baadhi kufungwa, matumizi duni ya uwezo, kutokuwa na uwekezaji zaidi, kushuka kwa mauzo ya nje na kupoteza ajira, mapato na fedha," alisema.

"Uchambuzi uliofanywa na CTI unaonyesha kuwa kuna angalau sheria 22 tofauti na kanuni 15 tofauti zinavyosimamia usindikaji wa chakula, nguo na mnyororo wa thamani wa dawa. Hii imesababisha mwingiliano wa kupita kiasi na kurudiwa kwa kazi za udhibiti zinazofanywa na wadhibiti kwenye biashara," alisema Dk. Kanje.

Alisema pia uchanganuzi wa CTI unaonyesha kuwa wafanyabiashara wanapata mizigo kama vile kutumia muda mwingi kuwahudumia wakaguzi wengi.

Aliongeza kuwa uchambuzi unaonyesha kuwa inachukua angalau siku 39 kusajili biashara na angalau siku 167 kutekeleza ambayo ni pamoja na kutokuwepo kwa muda wa kuwasikiliza wakaguzi, maandalizi ya nyaraka, kufuatilia masuala ya udhibiti na kuhudhuria mafunzo ya lazima.

"Athari za kanuni kwenye mnyororo wa thamani ni kubwa na inakadiriwa kuwa gharama za kutoa na wasindikaji wa chakula wakati wa awamu ya kuanza ni shilingi za Kitanzania 6,482,600 wakati gharama ya moja kwa moja ya kutoa kwa mwaka inakadiriwa kuwa Sh. 15,513,000 na makadirio ya gharama zisizo za moja kwa moja za kazi. , usafiri, mawasiliano na tija ya hasara inayofikia angalau Sh. 9,271,666," alisema.

Alisema hiyo ina maana kwamba jumla ya makadirio ya gharama ya kutoa (ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja) ni 31,267,266 kwa biashara moja kwa mwaka na kuongeza kuwa katika minyororo ya thamani ya nguo na dawa, inakadiriwa kuwa shilingi 67,378,666 zinatumika kama gharama ya kufuata kanuni kwa mwaka.

# Asasi za kiraia zataka mazingira bora ya kazi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MASHIRIKA 15 yasiyo ya kiserikali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, yanakusudia kufikisha mapendekezo yakiwamo ya kisheria, kisera na kiutendaji katika vyombo vya uamuzi likiwa ni pamoja na bunge na serikali, ili zifanye kazi katika mazingira mazuri na kuleta maendeleo nchini.

Hatua hiyo ni baada ya kujadili na kufanya uchechemuzi wa changamoto zinazotokea katika mashirika hayo, ikiwamo uboreshaji wa sheria na taratibu za ulipaji kodi na kujikuta yakifanya kazi katika mazingira magumu.

Kaimu Mkurugenzi wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) , Wakili MarkPhason Mshana, aliyasema hayo mjini hapa, huku akisema wamekutana na wadau hao ili kupitia maoni yaliyokusanywa kutoka kwenye asasi hizo nchini.

Wakili Mshana alisema kupitia Mradi wa URAIA WETU, unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), unaotekelezwa na asasi ya kiraia ya Foundation For Civil Society (FCS), unaangalia kuweka mazingira mazuri kwa asasi hizo kufanya shughuli zao.

Alisema mazingira yanayoangaliwa yapo katika maeneo matatu, ya kisera, kisheria na kiutendaji na kikubwa wanachotaka kupeleka katika vyombo vya uamuzi ni kutokana na asasi za kiraia kama muhimili wa sita wa shughuli za nchi, uweze kuwa na nafasi nzuri za kufanya kazi bila ya mikwamo.

"Tunakutana na wadau mbalimbali kutoka katika kila mkoa, na tumepata maoni mengi, hivyo tumeamua kukaa pamoja ili kukubaliana nini changamoto tuanze kufanya uchechemuzi," alisema Wakili Mshana.

Alisema malalamiko mengi ambayo yanatoka kwa wadau hao ni kuhusu kuwapo kwa sheria nyingi za asasi za kiraia, kuangalia sekta hiyo ambazo kuna wakati zinawachanganya ni sheria ipi wanatakiwa kufuata.

Alisema wanaangalia kuwa na sheria moja ambayo wataifuata asasi zote ili kila moja aweze kujua, anaifuata na kwa wakati mmoja.

"Ziko kodi kama za wafanyakazi, hizo hazileti changamoto, lakini changamoto ipo kwa zile shughuli ambazo asasi wanazifanya, lakini wanatozwa kodi, kwa mfano, wanapoagiza vifaa kwa ajili ya shughuli fulani unakuta zinatozwa kodi wakati asasi mara nyingi zinategemea ufadhili.




Naibu Kamishina wa Uhamiaji, Julia Sagamiko (wa nne kushoto) kwa niaba ya Kamishina, Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makalala, akikabidhi msaada wa mahitaji mbalimbali kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Julias Mwaisalage, jijini Dar es Salaam jana, uliotolewa na Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa wanaopata matibabu katika taasisi hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC Iringa awaonya wafanyakazi kuvujisha siri wakazi Vigwaza

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Kheri James, ameonya watumishi wa umma kuvujisha siri za serikali ikiwa ni pamoja na barua na kuwataka kufanya kazi kwa weledi huku wakizingatia kiapo walichokula kama watumishi wa umma.

Onyo hilo lilitolewa juzi wakati wa ufunguzi wa mafunzo maalum na vikao vya warsha kwa wataalam kutoka Chama cha Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu Tanzania (TRAMPA) Mkoa wa Iringa.

Akifungua mkutano huo, james aliwataka watumishi wa umma kuwa waaminifu katika maeneo yao ya kazi. Mkuu huyo wa wilaya alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba.

"Wataalam kutoka Chama cha Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu Tanzania wanatakiwa kuzingatia maadili ya kitaalamu, hususan katika kulinda siri za serikali na kufuata taratibu rasmi za kutoa taarifa," alisema.

Pia alisema serikali inatambua mchango wa taaluma ya usimamizi wa nyaraka na kumbukumbu kama chombo muhimu kinachosaidia kutambua changamoto za kijamii kwa ajili ya serikali kuingilia kati kwa wakati.

"Mafunzo haya yataongeza uwezo wenu na uweledi katika kutekeleza majukumu yenu katika ofisi ambazo kwa sasa mnafanyia kazi. Hata hivyo, nimearifiwa kuwa mafunzo haya yatakwenda sambamba na kiapo cha uadilifu. Nawasihi kila mmoja wenu aishi kwa kufuata kiapo ambacho kitatolewa.

"Nataka kuwakumbusha kwamba kutofuata kiapo si tu kukiuka sheria na kanuni bali pia ni dhambi kwa sababu unapochukua kiapo, unawaapia si tu serikali bali pia muumba wako," alisema.

Aliwasihi wataalam hao kuwa waaminifu wanapohitajika nyaraka na mamlaka nyingine, kuepuka kuchelewesha kuwasilisha nyaraka ili kuhakikisha haki inatendeka.

"Kama ukichelewesha kuwasilisha barua, haki inaweza kuchelewa, muhtasari wa mkutano fulani unaweza kuwa unahitajika kwa kumbukumbu ili kuhakikisha maamuzi yanafanyika kwa usahihi. Tuwe waaminifu, mnashikilia haki za watu, mnashikilia hatima za watu.

"Kwa kusema kuwa huwezi kupata barua ile, inaweza kuchukua muda mrefu, nawasihi muwe waaminifu na mpende kazi yenu," aliongeza. Aidha, aliwaomba viongozi wa serikali kuacha kuwachukulia waendeshaji wa rekodi kama wahudumu wa ofisi kwa sababu nao ni wafanyakazi kama wengine.

"Na kwa upande wetu viongozi, Katibu wa Jumuiya, tuheshimu taaluma hii. Tusimwone mwandishi wa rekodi kama mtu wa kutuma kuleta chai kwa wageni wanapokuja ofisini. Narejea, mwandishi wa rekodi siyo mhudumu wa ofisi wala mtu wa kutumwa kununua chai kwa wageni katika ofisi. Tuheshimu taaluma hii," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa TRAMPA, Devotha Mrope, alisema lengo la mafunzo haya ni kuongeza uwezo wao na kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

Aliongeza pia kwamba TRAMPA itahakikisha wanazingatia maadili na nidhamu miongoni mwa washiriki, katika eneo la kazi na nje, ili kudumisha viwango vya kitaaluma.

Mwenyekiti huyo alisema kaulimbiu ya mafunzo hayo ni "Msingi wa Maadili ya Usimamizi wa Nyaraka na Kumbukumbu: Uadilifu na Siri ni Nguzo za Taaluma."

Baadhi ya washiriki katika mafunzo hayo, Dorkasi Brown na Atha Jonathan Kasongo, walisema suala la uadilifu limekuwa changamoto kwa baadhi ya wataalam, na mafunzo haya yatasaidia kuziba pengo hilo.

## Jukwaa la viongozi lachangia milioni 13.7 waathirika Hanang

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi amepokea msaada wa Sh. milioni 13.7 kutoka kwa wanachama wa kundi la viongozi Tanzania, kwa lengo la kuwasaidia waathirika wa maafa Hanang.

Akipokea msaada huo juzi jijini Dodoma, Dk. Yonazi aliwashukuru wanachama wa kundi hilo kwa kujitoa kwao kwenda kwa waathirika wa maporomoko ya tope, mawe na magogo wilayani Hanang mkoani Manyara yaliyotokea mwishoni mwa mwaka 2023.

Dk. Yonazi alisema msaada huo pamoja na misaada ya wasamaria wengine inaunga mkono jitihada za serikali zinazoendelea katika kurejesha hali ya kawaida kwa waathirika hao, ikiwemo kujengea nyumba 108 ili waendelee kujitafutia riziki na kujiletea maendeleo.

"Tunawashukuru wenzetu wa kundi la Viongozi Tanzania kwa uzalendo waliouonyesha kwa ajili ya mchango huu mkubwa walioutoa, niwaombe Watanzania wenzangu tuzidi kushikana mkono hasa nyakati hizi ambako sehemu nyingi nchini kumetokea majanga mbalimbali, jambo jema kuendelea kushirikiana kuwasaidia ndugu zetu," alisema Dk. Yonazi.

Miongoni mwa wajumbe wa kundi hilo, Benjamin Thompson, na Mhandisi Archard Kato, walisema kundi hilo linaundwa na viongozi mbalimbali wa serikali, taasisi za umma, sekta binafsi, wahadhiri vyuo vikuu, vyama vya siasa na wana diaspora.

Thompson alisema michango hiyo ilikusanywa kutoka kwa wanachama 145 kati ya 600 walioko kwenye kundi hilo, ambao ndio waliweza kuchangia kwa wakati huo.

"Mkusanyaji wetu alikuwa ni Zamaradi Kawawa,ambaye alifanya kazi nzuri sana na kwa uaminifu mkubwa. Baada ya kumaliza kazi hiyo, tulikubaliana kwamba aweke pesa hizo kwenye akaunti ya maafa," alisema.

Naye Mhandisi Kato alisema wanachama wa kundi hilo wameguswa na janga hilo la Hanang na hivyo kuona umuhimu wa kutoa michango hiyo katika kuunga mkono juhudi za serikali za kukabiliana na majanga kama hayo.

"Tunaahidi kwamba tutaendelea kuisaidia serikali kwa kidogo tulicho nacho katika kukabiliana na athari za majanga kama haya, na tungependa kuona hili jambo linaenea kwa watanzania wengi, yaani hata kabla ofisi yako haijafika au serikali angalau watanzania wenyewe wawe wanafanya jambo la mwanzo kwa uzalendo wao katika kukabiliana na mambo ya dharula," alisema Kato.

Maafa ya maporomoko ya ardhi Hanang yalitokea Desemba 3, mwaka huu, Manyara na kusababisha vifo ya zaidi ya watu 80, huku mamia wengine wakiachwa bila makazi, pamoja na uharibifu mkubwa wa miundombinu.

# MAISHA

MEI 12, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

**Ngisi wa kukaanga na pilipili**



Ukurasa 14

## UREMBO:

Usitumie kemikali kuondoa ndevu



## HARUSI


Ukurasa 12



# Tumia ubunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo

Ukurasa 15

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA




| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| X | M | B | I | D | A | D | K |
| V | S | O | Z | N | F | Q | M |
| G | D | Y | E | J | H | R | O |
| I | F | A | M | I | L | Y | M |
| R | B | P | L | C | W | U | G |
| L | A | T | O | B | A | B | Y |


| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| J | ■ | K | U | N | D | I |
| A | ■ | ■ | ■ | D | ■ | M |
| M | ■ | F | A | A | ■ | B |
| B | A | A | ■ | Z | I | I |
| A | ■ | I | L | A | ■ | S |
| Z | ■ | D | ■ | ■ | ■ | H |
| I | G | A | W | E | ■ | A |

## AMSHA AKILI

HAYA WATOTO WAZURI. TUMSAIDIE NYUKI AKAFYONZE UA LAKE.




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MBU, TUA, BAA, GUU, CHAMA, IBAKI, TUMBA, ADABU, ASTAAFU, CHAGUZI

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa akitembea juu ya sakafu ya marumaru kwa mwendo wa haraka, mama yake alimwangalia na huku akiwa na hofu asije akateleza na kuanguka chini.

Mama: Grace unakimbilia wapi, hujui kama unatembea kwenye marumaru?

Grace: Mama nakwenda kuchukua kitabu changu cha hadithi Juma ameniibia.

Mama: Lakini kuwa mwangalifu, usije ukaumia na mimi sina pesa ya kukupeleka hospitali.

Grace: Lakini mama kule shuleni mwalimu alitufundisha kwamba 'kuteleza si kuanguka', hivyo sina hofu.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu alitaka kuwajenga muwe na ujasiri wa kufanya jambo ambalo awali umeshindwa.

SWALI

Taja aina tatu ya wanyama wa jamii ya swala wanaopatikana porini.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Vyanzo vya matatizo ya ndoa nyingi-2

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu ya vyanzo vya matatizo ya ndoa nyingi sehemu ya pili. Tayari wiki iliyopita tulianza kuona vyanzo kadhaa ambavyo nilivitaja na kuvichambua.

Kwa wale ambao hawakubahatika kusoma makala iliyopita, vyanzo nilivyotaja ni ndoa zilizofanyika pasipo Mungu kuhusika yaani wakati ukiwa adui wa Mungu, ukifuata zaidi mambo ya kidunia.

Chanzo kingine ni kupata mimba kwa bahati mbaya, pasipo kupangilia. Pia kujihusisha na kimapenzi kabla ya ndoa. Vile vile ndoa zilizofungwa baada ya mtu kwenda kwa mganga wa kienyeji.

Msomaji wangu, hebu sasa tuende zaidi tuangalie vyanzo vingine. Zipo ndoa zilizofungwa kwa shinikizo la wazazi. Hizi nazo zimekuwa mwiba katika familia nyingi.

Wako wazazi wenye tabia za kuwalazimisha watoto wao wajiingize katika ndoa mbaya (zisizo sahihi). Wazazi wengi wana shauku kubwa sana kuona watoto wao wakiolewa na kuoa. Wazazi wako wakikulazimisha ufunge ndoa, madhara utayapata wewe na siyo wao.

Kwa mfano, mzazi anapoona binti yake amesimama na vijana wenye muonekano mzuri (uwezo fulani wa fedha), huwa wana tabia ya kuhisi huenda kijana huyo anaweza kumfaa mtoto wao.

Hata kama binti huyo akijitetea na kusema kuwa mwanaume huyo hawezi kufaa, bado wao hulazimisha na kudai binti yao akishaolewa na huyo kijana ataweza kumbadilisha.

Chanzo kingine ni kulawitiwa au kubakwa wakati wa udogo. Katika mazingira haya, vijana wengi sana hutukanwa/hudhalilishwa kijinsia wakati wakiwa wadogo.

Hali hii imewasababishia watu wengi sana kupata madhara katika masuala ya mahusiano. Pia kuna roho ambazo huwavamia watu mara tu wanapobakwa, lengo likiwa kuvuruga hatma zao.

Chanzo kingine ni ndoa ambazo wahusika walishawahi kufanya agano la damu na mtu mwingine (agano la Amini). Vijana wengi sana hujiingiza katika maagano ya damu wakiwa na lengo la kuonesha kuwa wanawajali sana wachumba wao.

Kwa ujinga, hujikata kwa kiwembe na kuchanganya damu zao pasipo kufahamu madhara ambayo yangekuja kuwapata hapo baadaye.

Na madhara haya hufanya kazi kubwa sana kinyume chao pale wanapokuja kuolewa na mtu mwingine tofauti na yule waliyefanya naye agano kama hilo.

Wapo wengine hutamka maneno pasipo kufahamu kuwa kuna nguvu kubwa katika maneno ya vinywa vyao. Mfano mtu anaweka agano akisema, "Nitakuoa, na kama nikikusaliti, maisha yangu yatakuwa ya giza totoro na huzuni kubwa".

Ina maana mtu aliyefanya agano hili la damu na kutamka maneno mazito kama haya, siku akivunja tu agano hili, hatakaa awe na amani katika ndoa yake kabisa. Hivyo, yatupasa kuwa makini sana tunapoweka maagano kwani hicho ni kifungo!

Chanzo kingine msomaji wangu ni ndoa zilizojengwa katika misingi ya bora kuolewa au kuoa kuliko kuishi hivi hivi. Upo msemo, 'bora kuwa na mkate nusu kuliko kutokuwa na mkate kabisa.

Ndoa za aina hii mara zote zinakuwa na matatizo sana maana mtu wa namna hii anakuwa tayari ameshindwa kumtanguliza Mungu mbele ili amchagulie mume ambaye ni mapenzi yake.

Chanzo kingine ni ndoa zilizojengwa katika misingi ya bahati nasibu. Kuna watu wengi ambao wapo tayari kusema, "NDIYO" kwa mtu yeyote anayekuja kuwaomba wafunge naye ndoa, labda kwa sababu wanahisi wamesubiri kwa muda mrefu sana na kwamba umri unakwenda.

Watu wa aina hii huja na misemo ya namna hii, "mimi niko tayari kuolewa na mwanaume yeyote atakayenichumbia. Nikisubiri mtu aliyekusudiwa naweza kusubiria milele. Ngoja nijaribu huu uhusiano, huwezi kujua ninaweza nikafanikiwa"!

Aina hii ya kuchukulia masuala ya ndoa kama bahati nasibu inaweza kusababisha matatizo kwenye ndoa. Makusudi ya Mungu tokea mwanzo ilikuwa ni kuwaunganisha watu aliowakusudia katika agano la ndoa na si kwa kufanya bahati nasibu.

Aidha, zile ndoa zilizojengwa katika misingi ya muonekano wa nje. Ule muonekano hauwezi kukufanya uwe na ndoa ya kudumu. Mara zote uzuri wa mtu hupotea kadiri siku zinavyozidi kwenda mbele.

Wanawake wengi utasikia wakisema, "bado natafuta mwanaume, awe mzuri, mrefu. Na kama hana muonekano mzuri sitakubali anioe". Wiki ijayo nitamalizia vyanzo vingine. Una maoni? Kisa cha kimaisha?

***Tuma ujumbe 0715268581. Au Email: fwingia@gmail.com***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Zawadi zinavyosababisha maumivu ya mapenzi

MOJA ya vitu ambavyo huwa hakina kipaumbele sana katika uhusiano wa kimapenzi, ni kitu kinachoitwa zawadi.

Lakini ukweli ni kwamba zawadi ina maana kubwa sana katika mahusiano ya kimapenzi zaidi hata ya udhaniavyo.

Kama uko katika uhusiano ambao una matatizo, ambao hauendi sawa, naamini ulishawahi kujiuliza hili swali, nilikosea wapi?

Umejiuliza ni wakati gani mambo yalianza kuharibika mpaka kufikia hatua unapigwa kama mbwa au umekuwa mtu wa kuachwa tu kila siku?

Mwanzoni, mwenzi wako alikuwa anakupenda, anakujali, mnachati kwa ujumbe mfupi wa maandishi katika simu ya mkononi kila baada ya dakika 10. Mara nyingine mnahamia kwenye kupigiana simu mara mbili hadi mara tatu kwa siku lakini sasa anakaa hata wiki nzima hakupigii simu.

Hajakuacha lakini hakujali kabisa. Unajiuliza ulikosea wapi? Najua kuna makosa mengi na inawezekana ushachanganyikiwa kabisa kwa hili kwa kuwa sasa unampenda sana.

Leo ngoja nikufundishe kosa kubwa ambalo ulilifanya bila kujijua, wala kujua kuwa ni kosa.

Ingawa kwa wanaume lipo, lakini mara nyingi kosa hili hufanywa na wanawake. Najua ulikuwa hujui kama ni kosa ila inawezekana ndiyo sababu alibadilika.

Hivi unajua ni kosa kisheria wapenzi au wanandoa kunyang'anyana zawadi, baada ya kupeana wakati mapenzi yalipokuwa yamechanua?

Hili ni swali ambalo limekuwa likiwatatiza wengi kwa sasa hasa kutokana na mikinzano inayochomoza ndani ya mahusiano.

Ili kuona na kujua ukubwa wa tatizo kisheria, nimezungumza na wakili nguli nchini, Onesmo Olengurumwa kutoka Kampuni ya Uwakili ya Afritanza Attorneys. Moja ya maswali yangu kwake, ilikuwa kutaka kujua utata uko wapi na sheria inasemaje kuhusu hilo; na haya ni majibu ya kisheria.

Kwamba wakati wote wa ndoa, mwanandoa anaweza kumpa mwenza wake zawadi yoyote ile kama gari, nyumba na vinginevyo atakavyoona inafaa.

Lakini akishamkabidhi inakuwa tayari ni mali yake moja kwa moja. Na aliyetoa zawadi hiyo, kisheria hawezi kuirejesha tena au kudhani ni mali ya familia.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971; mwenye majukumu ya kisheria ya kutunza mwenzake kwenye ndoa ni mwanaume.

Mwanamume anapaswa kumlisha, kumvisha, kumtibu na kumjengea mke au wake zake isipokuwa mwanamke, atafanya tu pale ambapo mume atakapokuwa hawezi tena kufanya kazi kutokana na ajali au magonjwa au changamoto zingine.

Anakuheshimu lakini hakunyenyekei. Sasa dada zangu kosa kubwa nikuwa wakishapenda wananyenyekea, wanakubali kila kitu hata vitu vingine vya kijinga. Wanafanya hivyo si kwakupenda lakini wanaogopa kuachwa.

Hilo ndilo kosa, kumfanyia mwanamume kila kitu, kwa kuwa unaogopa kuachwa, ndiyo sababu utaachwa au utateseka katika uhusiano wako wote. Unachotakiwa kufanya ni kumheshimu lakini si kumuogopa wala kumnyenyekea.

Kama kitu huwezi kufanya mwambie hiki hapana, mwambie nakupenda ila hili hapana.

Kingine, Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 ya mwaka 1971 kama ilivyorekebishwa mwaka 2019, ni sheria kuu inayosimamia masuala ya ndoa nchini Tanzania.

Hata hivyo, sheria hii ni moja kati ya sheria kongwe nchini Tanzania na imekabiliwa na changamoto nyingi ambazo ni pamoja na; kuruhusu mazingira fulani ya ubaguzi wa kijinsia kwa wanawake na wasichana.

Kwa mfano, inawabagua wavulana na wasichana katika uwezo wa kuingia katika ndoa.

Pili, mnapaswa kujua Sheria ya Ndoa ina utata katika suala la ugawaji wa mali za ndoa wakati wa talaka hasa katika ndoa za mitala.

Vilevile, sheria hii inatoa wajibu kwa mume tu kutoa mahitaji kwa ajili ya familia, na imeshindwa kutoa tafsiri na adhabu juu ya masuala ya ukatili hasa wa nyumbani.

Upungufu na changamoto zilizomo katika sheria hii zinaleta mkanganyiko katika kusimamia na kutafsiri masuala yanayohusu ndoa nchini Tanzania.

Ni hivi! Unaweza kuona anacheka lakini kisaikolojia kila mwanaume anahitaji mwanamke ambaye anaweza kumuambia hapana.

Ni jambo la kisaikolojia kuwa wanaume, tunataka wanawake wanaojiamini, wasipopelekeshwa pelekeshwa wenye nidhamu, lakini sio mazuzu wanaofuata kila kitu.

• ***Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 715 545 490***

# HARUSI







Ni picha zilizojaa kumbukumbu nyingi kwa Abdallah Jeilan na mke wake Sophia Firoz Rashid, wakati walipofunga ndoa na kufuatia tafrija fupi katika ukumbi wa Ngome, Sinza jijini Dar es Salaam.





# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## YA KALE NI DHAHABU

UKWELI umedhihirika kwamba ya kale ni dhahabu! Usemi huo unaendelea kuthibitika katika dunia ya mitindo, kwani aina nyingi ya mavazi ya zamani, bado yanatamba na kupendwa na vijana wa kisasa.

Dhana hiyo inatokana na ukweli kwamba mitindo mingi ya magauni yenye umaarufu chanzo chake kinatoka katika taifa la Ugiriki ya kale.

Unapowaona wanawake wengi waking'ara kutokana na magauni marefu na yenye mitindo ya kushangaza, tambua kwamba warembo wa kipindi hicho walikuwa wakiyavaa.

Magauni yenye shingo za umbo la 'V' au sehemu kubwa ya maeneo ya magauni yapo wazi ni baadhi tu ya mitindo ya kale ya Kigiriki ambayo yanaendelea kupendwa hadi leo duniani kote.

Jamii ya Kigiriki ya kale waliwafanya wanawake kama pambo la asili, hivyo walitamani kuwaona kila wakati wakiwa wanang'aa na ndio maana nguo zao zilishonwa katika ustadi mkubwa.


Mitindo mingi ya magauni yanayovaliwa katika sherehe mbalimbali za harusi yamebuniwa katika mfumo wa Kigiriki.

Hata aina ya viatu vinavyovaliwa sasa ni matokeo ya wabunifu wa kale ambao kila wakati walitaka kumuona mwanamke akimeremeta mithili ya malaika.

UREMBO

Na Mary Geofrey

# Usitumie kemikali kuondoa ndevu



BADALA ya kuhangaika kutafuta dawa zenye kemikali kuondoa ndevu au vinyweleo usoni, kuna njia mbadala ambazo ukitumia hautapata madhara.

Hizi ni baadhi ya njia za asili unazoweza kutumia na kuondoa ndevu kwa urahisi ukiwa nyumbani kwako.

**PAPAI NA MANJANO**

Tengeneza mchanganyiko wa papai na manjano ili kudhibiti kuendelea kuota kwa ndevu na vinyweleo mwilini.

Chukua bakuli andaa vipande vinne vya papai,vijiko viwili vya unga wa manjano vichanganye vizuri upate uji mzito wa mchanganyiko huo kisha jipake mahali palipoota vinyweleo visivyohitajika.

Acha kwa dakika 20 hadi ukauke na kubakia mkavu kisha jibandue kwa kusugua ili kuzuia kuota kwa vinyweleo tena.

Kupata matokeo mazuri fanya hili zoezi mara tatu kwa wiki.

**LIMAO NA ASALI**

Kamua juisi ya limao changanya na asali vijiko viwili koroga hadi upate uji mzito kisha paka sehemu iliyoota vinyweleo na kaa kwa dakika 15 hadi20.

Kisha bandua kwa kusugua ili kuondoa nywele zilizopo na kudhibiti kuendelea kuota vinywele

Kupata matokeo mazuri fanya hili zoezi kila siku kabla hujaingia kulala

KITUNGUU THAUMU NA CHUMVI

Chukua punje kumi za kitunguu thaumu ziponde pamoja na kitunguu thaumu kisha jisugulie mahali penye vinyweleo na kaa kwa dakika 15 kisha nawa na maji safi na jikaushe kwa kitambaa

Kitunguu thaumu kinasaidia kuzuia kuendelea kuota kwa vinyweleo na kufanya ndevu na vinyweleo kupotea.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Ngisi wa kukaanga na pilipili

SAMAKI aina ya ngisi ana ladha tamu hasa wale walioandaliwa vizuri na kuwa laini.

Hata hivyo, ukiwa nyumbani unaweza kumuandaa ngisi na kufurahia maisha na familia yako.

Mahitaji

Ngisi nusu kilo, mafuta kupikia nusu lita, chumvi kiasi, juisi ya limao ama ndimu robo kikombe cha chai na pilipili kiasi.

Namna ya kutengeneza

Chukua ngisi wako na kisha muoshe vizuri na toa wino wake. Unaweza kumkatakata vipande kama utapendelea.

Muhifadhi katika sufuria au bakuli kavu.

Baada ya hapo umuinjike jikoni na kumwacha achemke vizuri ili kupata nyama laini. Baada ya kuiva opoa sufuria yako na weka pembeni.

Kisha chukua karai la mafuta na injika jikoni. Baada ya mafuta kupata moto tosa ngisi wako na acha wachemke na mafuta hadi wabadilike rangi.

Baada ya hapo ipua na weka pembeni.

Chukua pilipili zako na kisha zioshe vizuri. Weka katika sufuria yenye maji, weka chumvi kiasi.

Weka sufuria jikoni na acha zichemke hadi ziive .

Epua na kisha saga na weka chumvi kiasi. Miminia juisi ya limao katika mchanganyiko wako.



Baada ya hapo chukua ngisi wako uliokaanga na kisha kwenye bakuli weka chachandu yake anza kula.

***0621467710***

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# TUMIA UBUNIFU KUPANGILIA NYUMBA YA NAFASI NDOGO

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini, wanaishi katika nyumba za kupanga.

Kutokana na hali halisi ya familia za kiafrika, ni chache ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba yote ama kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo za kiafrika, nyingi huwa zinajumuisha zile kama zinavyojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended families', hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo ili kumudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia, lazima ubunifu na akili nyingi vitumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa samani katika nyumba hiyo ndogo, lazima uhakikishe unaweka zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano, meza ya televisheni, unaweza kuweka ambayo inakuwa na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu na kadhalika.

Tumia sehemu ya ukuta wako wa dari 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine kama mapambo na kama ni jikoni unaweza kujengea na kuweka vyombo na vitu vingine na likatumika kama kabati la kawaida la vyombo.

Kabla ya kutengeneza fenicha hizo, hakikisha kwanza umepima nafasi iliyopo na ni muhimu kuzingatia zaidi upangaji wa vitu vyako ndani uwe wa kutumia hesabu zaidi si kuweka ilmradi.

Epuka kuweka vitu hovyo ikiwezekana panga ambavyo una uhakika ni vya muhimu zaidi.

Kwa upande wa viti au sofa, hakikisha unaweka ambazo hazichukui nafasi kubwa, kabla ya kununua au kutengeneza ni vema ukapima nafasi ambayo umepanga kuziweka.

Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fenicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa na ikiwezekana ziwe ni nyembamba zenye nafasi ya kuelekea juu na si kwa upana.

Usiweke kitu ilimradi umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingatia umuhimu wake, na nafasi uliyonayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa fenicha, kumekuwapo na mabadiliko makubwa, pesa yako ndio inaweza kuamua uwe nayo ya dizaini gani.



## Huna sababu kukosa mboga nyumbani



UWE kwenye nyumba ya kupanga au ya kwako uliyoijenga mwenyewe, unaweza kabisa kula mboga za majani zilizo 'fresh' na salama zaidi.

Mtaalamu wa bustani, Janeth Augustino, anasema ni rahisi kuanzisha bustani ya mboga za aina mbalimbali nyumbani kwa kuwa ni mimea inayohitaji mwanga na jua kiasi.

Anasema tairi chakavu au chupa za maji ya kunywa, ni zana nzuri za kuanzisha bustani ya mboga nyumbani.

"Kwa mfano wakati huu wa mvua, mboga huwa zinaadimika sana kwa sababu nyingi zinalimwa kwenye mashamba makubwa ambako mkulima hawezi kuzuia hali ya hewa, ukiwa na bustani ya matairi kibarazani, unaweza kuzisogeza juani na kuzifanya zishamiri, wakati wa jua unazikinga kwa kuziacha kibarazani muda mwingi," anasema.

Jesca anasema tairi chakavu, viroba, chupa za plastiki au makopo ya kupandia maua yanaweza kutumika kutengeneza bustani hiyo.

Anasema: "Kwa wanaotaka kutumia vibaraza, matairi au makopo ni mazuri zaidi kwao, wanaoweza kutumia viroba wanatalazimika kuviweka chini pembeni ya uzio au nyumba, ni bustani nzuri inayokuhakikishia usalama na ubora wa mboga unazokula."

Anasema bei ya mbegu ya mchicha na aina nyingi za mboga inaanzia Sh. 500 na kwamba kwa bustani ndogo za vibarazani, mbegu za Sh. 500 zinatosha kwa kuanzia.

Anashauri kwamba bustani hizo hazihitaji kupulizwa dawa za kemikali na badala yake, majivu au maji ya majani ya mwaobaini yaliyochemshwa yanaweza kutumika kama kiuatilifu salama.

Anasema mkulima anaweza kutengeneza bustani ya vitunguu, matango au mboga.


# MATUKIO KATIKA PICHA



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akikagua gwaride la Jeshi la Polisi, kabla ya kufungua Kituo cha Polisi Daraja "A" Wilaya ya Kipolisi Mtumba na kukabidhi magari 21 kwa jeshi hilo, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa (kulia), akizungumza na wadau wa taasisi za kifedha nchini, baada ya kumaliza semina kuhusu mikakati ya kuongeza ushiriki wa Makandarasi na Washauri Elekezi kwenye miradi ya ujenzi iliyoandaliwa na Wizara hiyo kwa Wabunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: WU**



Msaidizi wa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Mbozi, Mkaguzi wa Polisi Kisbert Kapondo akifanya ukaguzi wa magari ya abiria katika eneo la Chimbuya, wilayani humo, mkoani Songwe juzi. **PICHA: ISSA MWADANGALA**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akishuhudia wakati Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Tulia Trust ambaye pia ni Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kulia), akikabidhi vyakula kwa Bibi Maligo Daimon, baada ya Waziri Mkuu kumkabidhi nyumba ya kuishi iliyojengwa na taasisi hiyo katika Mtaa wa Ilolo jijini Mbeya, jana. Kushoto ni Mke wa Waziri Mkuu, Mama Mary Majaliwa na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera. **PICHA: OWM**



Wananchi wakichagua viatu katika Mtaa wa Kongo, Kariakoo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Russia yateka vijiji Ukraine

**MOSCOW,** Russia

WIZARA ya Ulinzi ya Russia, imesema kuwa vikosi vyake vimedhibiti vijiji sita mashariki mwa nchi ya Ukraine.

Katika taarifa ya wizara hiyo kwenye mtandao wa Telegraph, ilieleza kwamba wanajeshi wamekomboa vijiji hivyo vya Borisivka, Ogirtseve, Pletenivka, Pylna na Strilecha katika mkoa wa Kharkiv, karibu na mpaka na Russia.

Mashambulizi kadhaa yaliyofanywa na Russia yamesababisha vifo vya watu wawili na wengine 16 kujeruhiwa mashariki na kaskazini mashariki mwa Ukraine.

Jeshi la Russia lilidai kutekwa kwa kijiji kikingine cha Otcheretyne, katika mkoa wa Donetsk.

Hivi karibuni vikosi vya Russia vilifanya mashambulizi ya kuvuka mpaka kuelekea mji wa Kaskazini Mashariki mwa Ukraine wa Kharkiv, hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya wizara ya ulinzi ya Ukraine na chanzo kimoja cha kijeshi.

Hata hivyo, taarifa ya wizara hiyo ilidai kuzuia mashambulizi hayo lakini mapigano makali bado yanaendelea na kwamba Russia imeanzisha mashambulizi ya angani karibu na eneo la mpakani.

Chanzo kingine cha ngazi ya juu ndani ya jeshi la Ukraine kilisema Russia ilipiga hatua kadhaa umbali wa kilometa moja kuelekea Ukraine na inajaribu kuzuia mashambulizi ndani ya eneo la nchi yake. **RFI**

**Hivi karibuni vikosi vya Russia vilifanya mashambulizi ya kuvuka mpaka kuelekea mji wa Kaskazini Mashariki mwa Ukraine wa Kharkiv, hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya wizara ya ulinzi ya Ukraine na chanzo kimoja cha kijeshi.**

# Marekani yakiri Israel ilitumia silaha vibaya

**WASHINGTON,** Marekani

RIPOTI mpya inaonyesha Marekani imekiri kwamba huenda Israel ilitumia silaha zilizotolewa na nchi hiyo zimetumika katika matukio yanayokwenda kinyume na sheria za kimataifa kuhusu haki za kibinadamu katika ukanda wa Gaza.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ilisema kuwa ni muhimu kufanya tathmini kuhusu matumizi ya silaha hizo ambazo zimetumiwa katika njia ambazo haziendani na majukumu ya Israel .

Ripoti hiyo ilieleza Marekani haikuwa na taarifa kamili katika tathmini yake na itaendelea kupeleka silaha nchini Israel kwa sasa.

Tathmini hiyo iliwasilishwa kwa bunge la Congress jana baada ya muda wake wa kutolewa kucheleweshwa.

Hata hivyo, Ikulu ya White House iliagiza uchunguzi huo ufanyike kuhusu jinsi taifa hilo na mengine sita yalivyotumia silaha zilizotolewa na Marekani tangu mwanzoni mwa mwaka.

**"Wakati wengi wenu mnawachukia Wayahudi, hamjali kwamba Wapalestina si wapenda amani, mnapaswa kuona aibu" alisema Erdan**

Ripoti hiyo ililaani wazi wazi kwa baadhi ya matukio yaliyofanywa na jeshi la Israel ndani ya Gaza, lakini haikutajwa moja kwa moja kwamba jeshi la Israel lilikiuka sheria za kimataifa.

Taarifa hiyo ilisema Israel ililazimika kukabiliana na changamoto ngumu za kijeshi ikiwa vitani na Hamas ndani ya ukanda wa Gaza.

Ilieleza kuwa Marekani ilipokea hakikisho kutoka kwa Israel kwamba ilifuata sheria za kimataifa ilipotumia silaha za nchi hiyo na kwamba taarifa hiyo ni ya kuaminika.

Wakati huo huo, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha kwa kura nyingi uamuzi wa kupanua haki za Palestina ndani ya shirika hilo na kuitaka ikubalike kuwa mwanachama.

Palestina imekuwa na hadhi ya mwangalizi asiyekuwa mwanachama tangu 2012, na haina baadhi ya haki za mwanachama kamili.

Hata hivyo, uanachama kamili unaweza tu kuidhinishwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Azimio hilo lilipitishwa juzi Ijumaa na litairuhusu Palestina kushiriki kikamilifu katika mijadala, kupendekeza ajenda na kuchagua wawakilishi wake kwenye kamati, ingawa haitakuwa na haki ya kupiga kura.

Hata hivyo, Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa,Gilad Erdan, alionekana kukasirishwa na hatua hiyo akisema chombo hicho kimekaribisha taifa la kigaidi katika safu yake.

Balozi huyo aliwakumbuka Waisraeli waliotekwa nyara na Hamas katika shambulio la Oktoba 7, mwaka jana na kusababisha watu 1,200 kuuawa.

Akihutubia mkutano huo wa Baraza Kuu, Erdan aliharibu nakala ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa na mashine ndogo ya kupasua karatasi, akiwashutumu wajumbe kwa kuharibu ahadi yao ya waraka wa kuanzishwa kwa umoja wa Mataifa kwa kupitisha azimio hilo.

"Wakati wengi wenu mnawachukia Wayahudi, hamjali kwamba Wapalestina si wapenda amani, mnapaswa kuona aibu" alisema Erdan

Balozi huyo alisema kwamba iwapo hatua hiyo itaidhinishwa, anatumai Marekani itapunguza ufadhili kwa Umoja wa Mataifa na taasisi zake. **BBC**



Raia wa Kipalestina waliopoteza makazi yao wakiwasili katika mji wa Khan Yunis baada ya kuondoka Rafah, kusini mwa Gaza jana. **PICHA: DPA**

# Labour kuufuta mpango kuwahamisha wahamiaji

**LONDON,** Uingereza

KIONGOZI wa Chama Kikuu cha upinzani cha Labour cha nchini Uingereza, Keir Starmer, amesema wataufuta mpango wa serikali wa kuwapeleka waomba hifadhi nchini Rwanda ikiwa wataingia madarakani.

Chama cha Labour kimeahidi badala yake kitaanzisha mkakati mgumu zaidi wa kukabiliana na wahamiaji wasio na vibali ikiwa ni pamoja na kuanzisha kikosi kazi kipya cha mpakani na kuongeza nguvu ya kupambana na ugaidi.

Kwenye hotuba yake aliyoitoa kwenye mji wa Dover, katika kaunti ya Kent, Starmer aliitaja sera hiyo ya Waziri Mkuu Rishi Sunak, kama hila na matumizi mabaya ya fedha.

"Tutaufuta mpango wa Rwanda. Niliwaambia hili tulipokutana mara ya mwisho wiki iliyopita. Unajua hiyo inamaanisha kuuondoa huo mpango kabisa, ndege na kila kitu. Hautafanya kazi. Ni kupoteza tu pesa na ni ulaghai,! alisema Starmer.

Alisema, ni watu wachache pekee walioondolewa, ambao ni chini ya asilimia moja ya wahamiaji wanaovuka bahari kwa kutumia boti ndogo kila mwaka.

Aliongeza kwamba Sunak anataka kuwaridhisha wenye misimamo mikali ya kihafidhina wanaopinga uhamiaji.

Starmer alisema hata mbunge wa chama chake cha Conservative katika eneo hilo, Natalie Elphicke ameungana na Labour akisema sera hiyo haifanyi kazi.

Zaidi ya watu 8,800 wameingia Uingereza kupitia bahari ya kaskazini mwa Ufaransa kuanzia mwezi Januari na kulingana na Starmer, watu 30,000 wameingia nchini humo mwaka 2023 kwa kutumia boti ndogo.

**DW**

MAKALA

# TUNALAUMIANA BURE KATIKA HILI



Na Magabilo Masambu

UPIGAJI hatua katika maendeleo ya nchi una uhusiano wa karibu na upunguaji wa wizi, ubadhirifu na ufisadi. Maana rahisi ni kwamba wizi ukikithiri, maendeleo yanapungua na ukiongeza maendeleo maana yake wizi na ufisadi uko chini. Wanaoiba inawezekana wanafanya maendeleo yao binafsi, wakati maendeleo ya taifa yanarudi nyuma.

Ni kweli kwamba wizi na ufisadi hauko Afrika pekee bali duniani kote lakini pengine tunazidiana kiwango na kasi ya wizi na ubadhirifu wa mali za umma. Hata hawa tunaowaona ni waaminifu na kwamba wamefanya maendeleo mpaka wanapata ziada ya kutusaidia, walituibia sana wakati tukiwa usingizini. Tulipofungua macho tukakuta wameondoka na mali zetu nyingi na historia ya ukoloni inaweka wazi. Hii ina maana kwamba hata majambazi wa leo wanaopora mali za watu binafsi au za umma, wanaonekana watu wa maana sana wanapotoa misaada kanisani au misikitini na mahali pengine.

Kwa nini tusilaumu? Kwanza tuna utamaduni kwenye jamii zetu za kiafrika hasa Tanzania ninayoijua kwa kiasi, wengine sijui sana wakoje. Tanzania katika mila na desturi zetu, katika baadhi ya familia, ikitokea bajeti imekuwa ndogo pengine kinachopatikana hakitatosheleza wanafamilia wote, basi baba au wakubwa wa familia ndio kipaumbele na watoto wanafuata.

Tulipokuwa wadogo tulikuwa tunafundishwa kula ugali kwa mchuzi, ukishiba ndiyo unapewa kafinyango kamoja ka nyama ili wakati unakwenda kucheza angalau na wewe uringishie wenzio kwamba kwetu walipika nyama. Ni kweli kwamba upande mmoja unamfundisha mtoto kubana matumizi kwamba kula nyama nyingi ni kumfundisha ufisadi na ulafi. Lakini upande mwingine yule mkubwa anaona anayo haki hiyo kwakuwa yeye ni mkubwa tafsiri yake ni kwamba, siku akishika madaraka atakuwa anajilimbikizia huku ikiwa kazi ngumu sana walioko chini yake kumkemea, kwa sababu tumeshazoeshwa wadogo kula kwa mchuzi huku nyama zikiliwa na wazee.

Mtoto naye akikua atakuwa hali mchuzi tena bali ni nyama kubwa kubwa tena zilizonona. Basi utaratibu unakuwa huo mpaka atakapoona kwamba ametosheka ndiyo anatoa salio kwa walioko chini kwa maana ya wananchi wa kawaida. Kumbe tunapaswa kufanyaje? Tuwafundishe watoto wetu kwa vitendo kutoka chini kabisa kwamba ikiwa baba huna pesa ya kununua kilo moja isiwe taabu nunua robo, gawaneni kwa jinsi hiyo watoto watajua kwamba kinapopatikana kidogo ni cha wote. Kwa hiyo akiwa kiongozi atajua kwamba hiki kinachopatikana chafaa kuwa kwa manufaa yetu sote.

Baada ya malezi ya nyumbani ni shuleni hapa ni pamoja na vyuoni. Hapa napo ni sehemu nyingine ya kufundisha na kujifunza ubadhilifu na wizi bila kujua. Shuleni na vyuoni ni sehemu muhimu sana ya kuwandaa viongozi wetu wa baadaye. Uzoefu na historia vinaonyesha viongozi wengi wa ngazi ya kitaifa, walianza kuwa viongozi katika taasisi za elimu hasa viongozi wa kisiasa, ukiachana na wale wanaoteuliwa.

Kwa hiyo kama nchi ni kuweka mifumo mizuri ya kuwapata viongozi kutokea huko ikiwa ni pamoja na kuwa makini kuhusu wageni maana wanaweza kujichomeka toka vyuoni kumbe wasiwe Watanzania.

Huko nako kuna kautamaduni kwamba mwanafunzi ambaye ni kiongozi mara nyingi amekuwa akichukuliwa tofauti na wengine. Mwanafunzi akishakuwa kiongozi tu tayari akilini mwake anaona anatakiwa kutazamwa tofauti. Wakati wa chakula tulikuwa na utaratibu wa kupanga mistari lakini viongozi wanaona hawana haki hiyo.

Jambo la pili ni kuhusu chakula chenyewe. Kiongozi anaona yeye anayo haki ya kupata chakula kingi zaidi kuliko wenzake (ulafi, ufisadi) eti kwa sababu ni kiongozi. Kwa hiyo yuko tayari wengine hata wakikosa yeye ashibe na ikiwezekana asaze.

Eneo lingine ni kuhusu makazi. Hawa wanafunzi kabla ya kuchaguliwa huwa wanaishi pamoja na wenzao tu na hakuna shida yoyote, lakini wakishachaguliwa tu, wanapewa maeneo yao rasmi. Ni kweli kwamba nia ni njema, lakini kinachotokea ni kwamba wakishapewa hayo makazi wao wanajiona ni daraja la juu zaidi kwa hiyo si watu wa kawaida tena na kwamba ukitaka kuwaona lazima uwe na ruhusa maalum!

Ndiyo maana leo baadhi ya viongozi ukiwa na tatizo kuwaona ni kazi ngumu sana. Huwezi kuamini kama ndio walewale vipindi vya uchaguzi wanakuna nazi na kusaidia kinamama ntilie kupika ubwabwa.

Mwisho, kama jamii tumebariki wizi na ufisadi. Tusipige kelele tuendelee kula matunda tunayoyapanda wenyewe, hivyo tusilaumiane mpaka tutakapobadili mifumo hii itengeneze watu wema badala ya majambazi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Urithi gani kuchukua vitu mlivyomnunulia marehemu?*



Na Adam Fungamwango

MAENEO ya Ilala jijini Dar es Salaam, aliishi mama mmoja ambaye pamoja na kubahatika kupata watoto, hawakuwa na uwezo wa kifedha.

Mama huyo alikuwa na kaka yake ambaye walizaliwa wawili tu, lakini alikuwa ameshafariki dunia.

Kaka yake alibahatika kupata watoto ambao wana uwezo kidogo wa kifedha.

Kutokana na kumpenda sana shangazi yao, ambaye walimwona kama vile marehemu baba yao, walimnunulia vitu vingi, vikiwamo vitanda, sofa, feni, kabati, redio, televisheni na samani kibao za ndani. Kwa bahati mbaya sana baada ya miaka mingi kupita yule, mama yule naye akafariki dunia.

Mazishi yakafanyika, lakini wakati wa mirathi, watoto wa kaka yake wakachukua kila kitu ambacho walimnunulia. Aliyenunua kitanda akachukua, wa televisheni akasomba, aliyempatia friji naye akaamua kuondoka nayo.

Wakubwa walipowauliza, wakawajibu kuwa walimnunulia wao, hivyo kwa sababu amefariki dunia basi wameamua kuchukua vitu vyao. Walipoulizwa watoto wa marehemu watarithi nini, wakajibu kuwa wanarithi vilivyobaki ikiwamo nyumba tu aliyojenga, na hao hawajawahi kumnunulia mama yao kitu chochote, pia shangazi yao hakuwa na uwezo wa kununua vitu vya gharama kama walivyonunua wao.

Ni binti mmoja ambaye alikuwa na hofu ya Mungu akakataa kuchukua chochote alichomnunulia shangazi yake. Akawaacha ndugu zake wafanye wanavyotaka kwa kuwa na yeye alipouliza alijibiwa kama walivyojibiwa wakubwa kwenye kikao cha mirathi.

Tukio hilo licha ya kuwaumiza watoto wa marehemu, lilimuumiza pia binti pekee wa ndugu wa waliofanya kitendo hicho.

Siku moja akakutana na mwanamuziki, TX Moshi William, na kwa kuwa wanafahamiana kwani ni mpenzi wa muziki wa dansi, hasa bendi ya OTTU jazz kama ilivyokuwa ikiitwa wakati huo, maarufu kama Msondo Ngoma na kumueleza kisa hicho.

Kama kawaida ya wanamuziki wa zamani, kisa hicho akakitungia mashairi na kupatikana wimbo uliitwao, 'Shangazi.' Ulirekodiwa kwenye studio za Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) katikati ya miaka ya 1990, ukieleza tukio zima jinsi lilivyokuwa.

Katika wimbo huu, mtunzi amechukua nafasi ya yule binti aliyekataa upuuzi wa kaka na dada zake wa kuchukua vitu walivyomnunulia marehemu. Tx Moshi aliimba kama ndugu anayewashangaa na kuwazodoa kwa kitendo walichokifanya. Mashairi yake ni haya hapa;-

"Wakati wa uhai wake, shangazi, alinunuliwa vitu vingi na kila mmoja wetu. Lakini cha kushangaza ni pale alipofariki shangazi yetu. Lakini cha kushangaza ni pale, alipofariki shangazi yetu.

"Wakati wa mirathi, kila aliyempa kitu, alikinyang'anya, walimwengu ni ya kushangaza, urithi gani huo, jamani eee, walimwengu ni ya kushangaza, urithi gani huo, jamani eee

"Wakati wa uhai wake, shangazi, alinunuliwa vitu vingi na kila mmoja wetu. Lakini cha kushangaza ni pale alipofariki shangazi yetu. Lakini cha kushangaza ni pale, alipofariki shangazi yetu.

"Kama ni lazima tungewauliza wenzetu wanavyofanya, kugawana mirathi. Walimwengu ni ya kushangaza, urithi gani huo, jamani eee, walimwengu ni ya kushangaza, urithi gani huo, jamani ee.

Nashangaa enyi ndugu zangu, mmebadilika na kutokwa na imani, mnavunja utu sababu ya mali hehe, tutasema nini eee, mbele za Mungu, he hehe.

Wakati wa uhai wake, shangazi, alinunuliwa vitu vingi na kila mmoja wetu. Lakini cha kushangaza ni pale alipofariki shangazi yetu. Lakini cha kushangaza ni pale, alipofariki shangazi yetu. Urithi gani huo, wa kunyang'anya mali."

Nadhani somo limeeleweka, kwani katika jamii yetu mambo kama haya ni mengi, na yanatokea katika staili tofauti.

Katika jamii ya Kiafrika, bado kuna matatizo pale linapokuja suala la mirathi, anapofariki yoyote yule.

Anapofariki dunia mwanamke, hasa kama yeye ndiye aliyekuwa mwenye mali, basi ujue baadhi ya ndugu watakuja juu na hawatotaka mume wake arithi mali.

Akifariki dunia mume, mdiyo kabisa, timbwili lake linakuwa si la kitoto kwa, mke ataanza kutesema masaa machache tu baada ya mwenzi wake kufariki.

Mke alipata taabu sana. Alilia kwa uchungu mara tatu. Kumpoteza mume, kutopata haki ya kumzika, lakini pia kunyang'anywa mali alizochuma na mume wake.

Kuna wale wanaotimuliwa kwenye kikao cha mirathi, yaani mke anaambiwa achukue nguo zake na watoto pia, mali zikibaki kwa ndugu.

Kusema kweli hii ni tabia mbaya sana, na kama ni mila, basi ni moja kati ya zile mila potofu.

Mtu anahangaika na mkewe, wanalala chini, wanajinyima na kula ugali, mlenda dagaa, ili wajenge na kununua vitu mbalimbali ambavyo vinawafanya kufurahia maisha.

Inakuwaje mume akifariki, ndugu ambao hawajui hata vimenunuliwa lini na wapi, wanakuja kuvishikilia na kujifanya vya kwao? Mbona na wao wana familia na hakuna anayewaingilia.

Ikumbukwe kuwa kila mmoja ana familia aliyoijenga, hivyo urithi utatoka kwenye familia yake, kwa nini watu wanataka kwenda kurithi vitu vya mtu mwingine? Hata kama ni ndugu yake mmezaliwa baba na mama mmoja, lakini ana mke na watoto ambao ndiyo wanatakiwa waupate.

Ukishangaa ya Mussa utaona ya Firauni, hawa nao waliochukua vitu walivyomnunulia shangazi yao, ni kiboko. Urithi gani huo wa kunyang'anya mali ambazo walimnunulia wenyewe?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam.
Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia.
Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa.
Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi.
Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Vipi umeletewa taarifa ambayo si nzuri?" Akaendelea kuuliza. Akahisi kuwa huenda amepata meseji au simu ambayo si nzuri. Bado hakujibiwa. Badala yake hali ilionekana kuwa mbaya kwa Nuru.

Alionekana kama mtu aliyefura kwa hasira, lakini pia jasho lilionekana kumtoka licha ya kwamba kulikuwa na feni ilimpepea. Macho yalikuwa yamemtoka pima mithili ya mtu aliyepigwa kabali.

Kila sekunde zilivyozidi kwenda ndiyo hali yake ilizidi kuwa mbaya akiasi cha kumtisha Heri.

Alionekana kama anataka kusema kitu lakini alishindwa. Ni kama kuna kitu kimekaba kooni.

Heri hakuamini alichokiona. Mtu ambaye walikuwa wanaongea na kucheka, amebadilika ghafla.

Aliwahi kusikia hadithi nyingi za wanawake au wanaume wanaofia kwa wapenzi wao. Akaona leo yamemkuta. Alichoona sasa ni kama Nuru anataka kutoka kitandani pale kumvamia, huku akitoa mikoromo ya kutisha.

Kwa mbali jasho la woga lilianza kumtoka. "Mtoto wa watu wakumbwa na nini tena?" Akajiuliza moyoni.

Mikoromo iliongezeka, na sasa Nuru alianza kutetemeka kama vile mtu aliyepigwa na baridi kali.

Macho yake yaliyobadilika na kuonekana ya kutisha na bado yaliendelea kumtazama Heri.

Mambo yakabadilika. Badala ya kumuonea huruma mgeni wake, akaanza kuingiwa woga yeye mwenyewe kuhusu usalama wake.


Kwa jinsi alivyokuwa, Heri hakuthubutu hata kumsogelea karibu, achilia mbali kumgusa.

Ni kipindi ambacho sasa aliona usalama wake ni muhimu zaidi kuliko kitu kingine chochote, kwani mgeni wake ananekana kubadilika na kuwa na sauti kama mnyama wa kutisha.

Akakumbuka kuwa mlango uko wazi. Akaanza kunyata kwa uangalifu. Kila akimuangalia ni kama mtu ambaye anataka kumrukia. "Kwa sababu gani?" Akajiuliza bila kupata jibu.

Alipopiga hatua tano za kunyata na kukaribia mlango, alikurupuka na kutoka nje mbio.

Alipofika kwenye mlango mkubwa akatazama nyuma kama anafuatwa. Hakumuona yoyote. Akapunguza mwendo. Akasimama na kufungua mlango mkubwa ambao wenyewe wanauita geti, akaanza kutembea taratibu kama hakukutokea chochote.




**"Mmmh!" Mama mmoja akaguna. Alionyesha kuwa anaishi mle ndani na ana uhusiano naye. "Katoka muda mrefu tu, wala hajatuaga, sijui kaenda wapi!"**

Baada ya kutembea umbali mrefu akasimama na kujiuliza anakwenda wapi? Akili ikamrudia kuwa ndani ya chumba chake amemuacha mtu. Na hayupo kwenye hali ya kawaida. Licha ya kuhitaji msaada, lakini mwenyewe anahitaji arejee nyumbani kwake kuendelea na maisha yake.

Hawezi kufanya hivyo kama mtu aliyekuwa ndani hajatoka. Pia kama likimtokea tatizo yeye ndiye atakayepewa lawama, atawajibika, kukamatwa na kupelekwa kwenye vyombo vya sheria, kama litamkumba baya zaidi lenye kuathiri afya yake.

Akili yake ilifanya kazi haraka haraka kuwaza nani anaweza kumsaidia kuhusu jambo lile. Haikumtuma kumtafuta rafiki yake yoyote yule kijana. Kesi iliyo ndani kwake, alihitaji mtu mwenye umri mkubwa mwenye busara, aliyeona mengim ambaye anaweza kumsaidia kwa mawazo, au kuwasiliana na watu ambao wanaweza kumaliza tatizo na yeye kutoingia matatizoni.

Aliona lolote litakalotokea kama akiwasiliana na mtu wazima wanaweza kuwa watetezi kwake.

Awali alitaka kwenda kwa mjumbe. Baadaye akatupilia mbali wazo hilo. Akamkumbuka mzee mmoja nyumba ya nne kutoka anapoishi. Anaitwa mzee Raia. Ni mzee mcheshi anayezoeleka kirahisi. Hata yeye amezoeana naye sana. Kila anapokutana naye, huwa anamtania na kumuomba hela kidogo ya kununulia tumbaku na ugoro.

"Enhee huyu huyu mzee ngoja niende kwake." Akajiambia mwenyewe, ingawa alijua familia yake itashangaa kwa sababu ni mara ya kwanza itakuwa kufika kwake.

Kutokana na shida kubwa aliyonayo wakati ule, aibu aliiweka pembeni. Akaongoza kiguu na njia hadi nyumbani kwa mzee huyo.

Aliwakuta baadhi ya kinamama nje, wengine wakipiga stori, mmoja akimsuka mwenzake. Tayari ilishatimu saa 12:30 jioni, kwa mbali giza lilishaanza kuingia.

"Shikamooni." Akasalimia. Wakamwangalia kwanza, halafu wawili wakaitia ," marahaba." Mmoja akaongeza, "karibu." "Ahsante." Akajibu kwa aibu kwa sababu hakuna hata siku moja aliyofika hapo. Wengine walikuwa wakifananisha na wengine hawamfahamu kabisa.

"Nimemkuta mzee Raia?" Akauliza. "Mmmh!" Mama mmoja akaguna. Alionyesha kuwa anaishi mle ndani na ana uhusiano naye. "Katoka muda mrefu tu, wala hajatuaga, sijui kaenda wapi!"

Heri akaishiwa pozi. Hakujua afanye nini. Na mpaka wakati huo hakujua aliyemuacha nyumbani ana hali gani. Na mle ndani kukoje?

"Akija tumwambie nani?" Akashtuliwa na swali kutoka kwa mama aliyemjibu kuwa hayupo.

"Hapana, nitakuja tena baadaye kumuangalia!" Akajibu kwa unyonge kabla ya kugeuka na kutaka kuondoka kama mtoto aliyenyimwa chakula.

"He! Huyoo, anarudi, una bahati." Sauti ilipenya masikioni mwake. Alikuwa amegeuka na kutaka kuondoka, lakini hakumuona mzee Raia aliyekuwa mbele yake, akirejea nyumbani.

Akageuza kichwa nyuma ili kumuangalia anayesema kuwa mzee Raia anarejea.

"Mzee wako uliyekuwa unamuulizia huyo hapo." Akasema tena. Safari hii alipogeuka alimuona. Alikuwa hatua chache kutoka mbele yake.

"Kijana leo iko mitaa ya nyumbani kwangu, karibu sana, maana kila mara tunakutana mitaani huko!" Kama kawaida mzee Raia alianza ucheshi wake.

"Ahsante mzee, shikamoo." "Marahaba, karibu ndani, maana naona baraza limetekwa na kina mama."

"Hapana mzee mimi siyo hata mkaaji." "Lakini naona kama ulikuwa umekuja nyumbani kwangu hivi!" "Ndiyo. Nimekuja kwako, nina shida, ila siyo ya kukaa ndani. Nakuomba twende pembeni kidogo tuzungumze mara mmoja."

Mzee Raia alihisi kabisa kuwa kijana ana shida kubwa. Kwa sababu hakuwahi hata siku moja kumuona anafika nyumbani kwake. Pili kwa jinsi alivyomuangalia tu usoni, alionekana kuwa na wasiwasi hivi. Kule kumwambia waende chemba kuzungumza, ina maana ni neno ya siri na lipo tatizo.

Heri hakubakisha chochote. Alimwambia kila kitu kama vile mtuhumiwa anavyomuweka wazi wakili wake ili ajue wapi kwa kuanzia kumtetea hadi mwisho wa kesi. Wakili hatakiwi kudanyangwa. Kudanganywa kunaweza kumfanya akashindwa mbinu za kumtetea mteja wake. Unapomwambia ukweli hata kama umetenda kosa, ana mbinu za kiufundi, mbali na elimu yake jinsi ya kumuondoa mteja wake shtaka.

"Duh! Pole sana kijana. Hiyo ndiyo dunia. Haya mambo yapo kwenye maisha. Sasa unaanza kukomaa kijana. Umeanza kuwa mwanaume." Akaongea mzee Raia huku akitabasamu.

Hali hiyo limshangaza Heri. Wakati yeye akiwa na hofu kubwa, lakini mzee Raia alionekana kama kulichukulia jambo hilo poa.


"Hivi huyu mzee hajamuona Nuru hali yake nini?" Akauliza kimoyomoyo.

"Sawa, hebu twende nyumbani kwako tukaangalie hiyo hali, halafu tuone tunafanyaje."

Kitendo cha mzee Raia kukubali kirahisi hivyo, licha ya kile alichomueleza kikionekana kwa cha kutisha, kilimfariji Heri.

Kwake ilionekana ni kama vile nusu nzima ya tatizo zimeshatatulika. Na kwa jinsi alivyoona mzee alivyolichukulia. Hakuonekana kupaniki, kwake ilionekana ni uamuzi sahihi alioufanya kwenda kumuita mzee huyo.

**Itaendelea Jumapili**



# BIERBER AWAJIBU KIVITENDO

MASHABIKI wa mwanamuziki maarufu wa Pop kutoka Marekani, Justin Bieber, wamefurahia tangazo lililotolewa na msanii huyo kwamba yeye na mkewe Hailey wanatarajia kupata mtoto wao wa kwanza.

Wanandoa hao awali waliripotiwa kuwa wanataka kupeana talaka, lakini ghafla uvumi huo uligeuka baada ya Bieber kuchapisha picha akiwa na mkewe wakifurahia maisha.

Taarifa zinaeleza kwamba Hailey ana ujauzito wa miezi sita.

Afya ya Bieber imekuwa katika mjadala wa kila siku kwa mashabiki wake, lakini ujio wa mtoto huyo umeleta ahueni kwa taarifa mbaya zilizokuwa zikiwazunguka wanandoa hao.

## JAIVAH ATAKA BIFU LIENDELEE

MKALI wa muziki wa Amapiano, Jaivah, amesema hana wasiwasi na malumbano kati ya watayarishaji wawili maarufu wa muziki Abbah Process na S2Kizy, kwa hakuna anayeumia.

Amesema tangu malumbano hayo yaanze hakuna mtu aliyedhurika wala mtu kutoka damu, hivyo wanaweza kuendelea kwa kuwa inaleta changamoto za kibiashara kati yao.

"Wote ni ndugu zangu kama hakuna mtu atakayetoka damu, sina matatizo na ugomvi wao jambo la msingi ni kuona unaongeza chachu katika kuongeza ubora wa kishindani," amesema.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TEN HAG BADO YUPO

KLABU ya Manchester United haina nia ya kumfukuza kocha, Erik ten Hag kabla ya fainali ya Kombe la FA mnamo Mei 25. ***(Telegraph)***

### TUCHEL AITAKA UNITED

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel ana nia ya kuwa kocha wa Manchester United iwapo klabu hiyo itaamua kumfukuza Erik Ten Hag. ***(Telegraph)***

### MOURINHO NAE AITAKA

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho angependa kurejea kwa kipindi cha pili lakini klabu hiyo haitaki kumteua tena Mreno huyo mwenye umri wa miaka 61, ambaye alitimuliwa na Roma Januari. ***(Manchester Evening News)***

### GUEHI KUUZWA

KLABU ya Crystal Palace iko tayari kumuuza mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 23, badala ya kumtoa winga wa Ufaransa Michael Olise mwenye miaka 22, au winga wa Uingereza Eberechi Eze mwenye miaka 25, msimu huu. ***(Givemesport)***

### GASSOVA ATAKIWA

WEST Ham imeanza mazungumzo ya kumsajili winga wa Corinthians mwenye umri wa miaka 19 raia wa Brazil, Wesley Gassova, ambaye pia analengwa na Liverpool. ***(Standard)***

### CHELSEA KUMPIGA BEI BROJA

CHELSEA inatafuta mnunuzi wa mshambuliaji wa Albania, Armando Broja kufuatia kipindi cha mkopo cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 na Fulham. ***(Fabrizio Romano)***

### WILLIAN AWINDWA DARAJANI

CHELSEA upo kwenye mazungumzo ya kumsajili winga, Estevao Willian mwenye umri wa miaka 17 kutoka Palmeiras . ***(Mail)***

### PICKFORD ALENGWA

CHELSEA pia wamemtambua mlinda mlango wa Everton, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 30 kama wanayemlenga majira ya joto. ***(Football Insider)***

### KELLY HUYO NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25. ***(Foot Mercado)***

### LEWIS HALL ALENGWA

MLINZI wa kushoto wa Newcastle United, Lewis Hall mwenye miaka 19, ameibuka kama nyota anayewindwa na Borussia Dortmund msimu wa joto. ***(Givemesport)***

### LAPORTA AMTAKA GREENWOOD

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amewasiliana na Getafe kuhusiana na hali ya mshambuliaji wa Manchester United Mwingereza anayecheza kwa mkopo, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 22. ***(Radio Marca)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WAGONGA NYUNDO KUMNG'OA WESLEY

● ● ● Ni kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho kwa ajili ya msimu ujao baada ya kocha....

**LONDON, England**

BAADA ya kuthibitisha wataachana na kocha wao kutoka nchini Scotland David Moyes mwishoni mwa msimu huu 2023/24, imefahamika kuwa Uongozi wa Klabu ya West Ham United umepanga kukiimarisha maradufu kikosi chao chini ya Benchi jipya la Ufundi litakalotangazwa baadae.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kuwa, Uongozi wa klabu hiyo umedhamiria kufanya hivyo, ili kuwa na kikosi imara kwa msimu ujao 2024/25.

Mchezaji wa kwanza anayetajwa kuwindwa klabu hapo kwa mujibu wa gazeti hilo ni kinda kutoka nchini Brazil na Klabu ya Corinthians Wesley Gassova Ribeiro Teixeira 'Wesley'.

Thamani ya Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 19 inatajwa kufikia Pauni Milioni 21, lakini inadaiwa kuwa tayari Uongozi wa Corinthians umeanza kuiwekea ngumu West Ham.

Gazeti hilo limeandika: "West Ham United inajipanga kumsajili Kinda wa Klabu ya Corinthians Wesley, kama sehemu ya harakati za klabu hiyo kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao 2024/25.

"Mail Sport inaelewa kuwa wawakilishi wa 'The Hammers' walimfuatilia Kinda huyo wakati wa mchezo wa ufunguzi wa msimu wa Ligi Kuu ya Brazil 'Serie A' mwezi uliopita ili kujiridhisha.

"Wesley, ambaye anaweza kucheza kama Kiungo Mshambuliaji ama Mshambuliaji wa kati, thamani yake inatajwa kufikia Pauni Milioni 21 na tayari uongozi wa klabu ya Corinthians umeanza kuiwekea ngumu West Ham.

# MBAPPE ATANGAZA RASMI KUONDOKA PSG

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe ametangaza kuondoka PSG mwishoni mwa msimu huu ambapo anatarajiwa kujiunga na Real Madrid.

Tangazo hilo linaileta Real Madrid karibu kumaliza harakati zao za miaka mingi za kumtafuta mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora katika kandanda duniani.


PSG itamenyana na Toulouse kwenye Uwanja wa Parc des Princes leo Jumapili, ambao utakuwa mchezo wa mwisho wa Mbappé wa nyumbani.

Mchezo wake wa mwisho kwa klabu hiyo umepangwa kuwa fainali ya Kombe la Ufaransa dhidi ya Lyon mnamo Mei 15.

Alisema katika video iliyotumwa kwenye Instagram: "Halo watu wote, ni Kylian. Nilitaka kuongea nanyi. Nimekuwa nikisema kwamba nitazungumza nanyi muda ukifika na hivyo nilitaka kuwatangazia wote.

"Sitaongeza muda na mchezo huo utakamilika baada ya wiki chache. Nitacheza mchezo wangu wa mwisho katika Parc des Princes Jumapili.

"Ni hisia nyingi, miaka mingi ambapo nilipata nafasi na heshima kubwa kuwa mwanachama wa klabu kubwa ya Ufaransa, moja ya klabu bora zaidi duniani ambayo iliniruhusu kufika hapa, kuwa na uzoefu wangu wa kwanza katika klabu na shinikizo nyingi, kukua kama mchezaji bila shaka, kwa kuwa pamoja na baadhi




ya wachezaji bora katika historia, baadhi ya mabingwa wakubwa, kukutana na watu wengi, kukua kama mtu na utukufu wote na makosa niliyofanya."

Mbappé aliwashukuru makocha wote watano ambao wamemsimamia PSG kwa nyakati tofauti, Unai Emery, Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Christophe Galtier na Luis Enrique -- pamoja na wakurugenzi wa michezo wa klabu hiyo.

Aliongeza: "Licha ya kila kitu kinachoweza kutokea nje, kelele hizi zote za vyombo vya habari vinavyozunguka klabu wakati mwingine, kuna baadhi ya wapenzi wa klabu ambao wanataka kuilinda na kuifanya ing'ae.

"Ni ngumu, na sikuwahi kufikiria kuwa itakuwa ngumu hivi kutangaza kwamba, kuiacha nchi yangu, Ufaransa, Ligue 1, michuano ambayo nimekuwa nikiijua siku zote lakini nadhani, nilihitaji hii, changamoto mpya, baada ya miaka saba. "

Vyanzo viliiambia ESPN kuwa Mbappé anatarajiwa kujiunga na Madrid, baada ya kufanya mazungumzo na klabu tangu angalau Februari.

Mnamo 2017, baada ya kutoka Monaco, Mbappé alikaribia kujiunga na Madrid, lakini alichagua PSG badala yake baada ya klabu hiyo kukubaliana mkataba wa rekodi ya dunia kwa kijana, wenye thamani ya euro milioni 180.

Mbappé aliendelea kuwa nahodha wa klabu ya PSG na mfungaji bora wa muda wote akiwa na mabao 255, akishinda mataji sita ya Ligue 1 katika misimu saba.

Katika kiwango cha kimataifa, alishinda Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa mwaka 2018 na alifunga 'hat trick' katika kushindwa kwao fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Argentina miaka minne baadaye.

# Arteta yupo hatarini Ligi Kuu England

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta huenda akakosa mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu England dhidi ya Everton.

Arsenal inakwenda jino kwa jino na Manchester City kwenye mbio za kufukuzia ubingwa na kinachoonekana vita itakwenda hadi mwisho wa msimu.

Arsenal ipo kileleni kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya Man City iliyopo kwenye nafasi ya pili, lakini yenyewe imecheza mechi moja zaidi, hivyo kupata ubingwa wanaomba wapinzani wao wateleze kwenye mechi tatu walizobakiza.

Kocha Arteta ni muhimu kweli kuwapo kwenye benchi la ufundi hasa kama wanataka kufanya vizuri kwenye mechi zao mbili zilizobaki kwenye msako huo wa ubingwa. Arsenal itasafiri kwenda kucheza na Manchester United, leo Jumapili huko Old Trafford, kabla ya kuwakabili Everton uwanjani Emirates.

Hata hivyo, Arsenal inaweza kumkosa Arteta kwenye benchi lake katika mechi ya mwisho ya msimu dhidi ya Everton kama atatenda kosa la kinidhamu kwenye mechi dhidi ya Man United na kuoneshwa kadi ya njano.

Kocha huyo kutoka nchini Hispania ameshaonyeshwa kadi tano za njano, hivyo kama ataonyeshwa moja zaidi basi atalazimika kuwa nje ya uwanja kwa mchezo mmoja.

Arteta aliwahi kukosa mechi moja kutokana na adhabu hiyo, ambapo alikosa katika mchezo wa kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Aston Villa, Desemba mwaka jana.

Makocha wa Ligi Kuu England wanaadhibiwa kila wanapooneshwa kadi tatu za njano na Arteta ameonekana kuwa ni mkosefu wa nidhamu kwa kiasi kikubwa msimu huu, ambapo hadi sasa ameshaonyeshwa kadi tano za njano.

Alioneshwa kadi za njano kwenye mechi dhidi ya Fulham, Luton na Brighton, na kwenye mechi zote mbili alizocheza dhidi ya Chelsea.

Hivyo, kwenye mchezo wa Man United uwanjani Old Trafford anapaswa kuwa mtulivu kwa kuwa akionyeshwa kadi ya njano, itamgharimu kwenye mechi ya mwisho.

# Casemiro, Richarlison watemwa Brazil

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

KOCHA wa Brazil, Dorival Junior amemjumuisha Endrick katika kikosi chake cha wachezaji 23 kwa ajili ya Copa America huku fowadi wa Arsenal Gabriel Jesus, Richarlison wa Tottenham na kiungo wa kati wa Manchester United Casemiro wakiwa miongoni mwa waliotemwa kwenye kikosi hicho.

Dorival pia alithibitisha kwamba Richarlison alikosa kucheza kikosi baada ya kupata jeraha la mguu akiwa na klabu yake.

Mshambuliaji chipukizi wa Palmeiras Endrick, ambaye atajiunga na Real Madrid aling'ara katika michezo miwili ya mwisho ya Brazil mwezi Machi.

Endrick mwenye, 17, alifunga bao lake la kwanza akiwa na Brazil katika ushindi wa 1-0 dhidi ya England Uwanja wa Wembley kabla ya kufunga bao katika sare ya 3-3 na Hispania katika mechi za kwanza za Dorival kuongoza.

Brazil wanamkosa mfungaji wao wa muda wote Neymar, ambaye hatashiriki michuano hiyo kutokana na jeraha la goti.

Wachezaji wawili wa Real Madrid Vinícius Júnior na Rodrygo, ambao wamechangia pakubwa kwa Madrid kushinda LaLiga na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wanatarajiwa kuongoza safu ya ushambuliaji.

Vinícius ni mshindani wa Ballon d'Or mwaka huu lakini Dorival alisisitiza: "Hatuhitaji nyota mmoja, nadhani mgawanyo wa uwajibikaji utasaidia timu kukua. Ni vizuri kuwa na wachezaji wa kiwango hicho."

Mshambulizi wa FC Porto, Evanilson ameitwa kwa mara ya kwanza huku Sávio akituzwa kufuatia msimu mzuri akiwa Girona kwa mkopo kutoka Troyes.

Wakati huohuo, Casemiro amepoteza nafasi yake kwenye kikosi baada ya msimu mbaya akiwa na Manchester United.

"Anastahili heshima yetu sote," Dorival alisema kuhusu kiungo huyo mkongwe. "Nilifanya mazungumzo naye huko Manchester miezi mitatu iliyopita. Anajua ninachofikiria kumhusu."

Dorival athibitisha kuumia kwa Richarlison

"Richarlison ana jeraha la mguu. Bado haijawekwa rasmi na klabu, lakini tuliwasiliana na mchezaji huyo na akatufahamisha." Mchezaji wa Aston Villa, Douglas Luiz ni mmoja wa wachezaji tisa wanaocheza Ligi Kuu waliojumuishwa kwenye kikosi cha Dorival.

Brazil ilishinda ubingwa wa michuano hiyo mara ya mwisho mwaka 2019.

Kwa sasa wanapambana kutafuta tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia kutoka ukanda wa Amerika kusini.

Brazil wako katika nafasi ya sita kwenye msimamo baada ya kushinda mechi mbili pekee kati ya sita za kufuzu na kushindwa mara tatu, matokeo ambayo yalipelekea Dorival kuteuliwa Januari.

Brazil itacheza mechi mbili za kujiandaa na mechi dhidi ya Mexico Juni 8 mjini Texas na dhidi ya Marekani siku nne baadaye mjini Orlando kabla ya kuanza mchuano dhidi ya Costa Rica Juni 24. Kikosi cha Dorival pia kitamenyana na Paraguay Juni 28 na Colombia Julai 2. katika Kundi D.

Kikosi kamili:

Makipa: Alisson Becker (Liverpool), Éderson (Manchester City) Bento (Athletico-PR);

Mabeki: Danilo (Juventus), Yan Couto (Girona), Guilherme Arana (Atlético-MG), Wendell (FC Porto), Beraldo (Paris Saint-Germain), Marquinhos (Paris Saint-Germain), Gabriel Magalhães (Arsenal), Militão (Real Madrid)

Viungo: Andreas Pereira (Fulham), Bruno Guimarães (Newcastle), Douglas Luiz (Aston Villa), João Gomes (Wolverhampton), Lucas Paquetá (West Ham)

Washambuliaji: Endrick (Palmeiras), Martinelli (Arsenal), Evanilson (Porto), Raphinha (Barcelona), Rodrygo (Real Madrid), Savinho (Girona), Vinícius Júnior (Real Madrid).

HABARI MICHEZO

# COASTAL YANUSA KOMBE LA SHIRIKISHO AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 2-0 ilioupata juzi kwenye uwanja wake wa nyumbani Mkwakwani jijini Tanga dhidi ya Singida Fountain Gate, umeifanya Coastal Union kukaribia kabisa kukata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Mabao ya straika anayecheza kwa mkopo akitokea Yanga, Crispin Ngushi dakika ya 26 na Greysan Gwalala dakika ya 46, yameifanya timu hiyo kufikisha pointi 37, ikikamata nafasi ya nne na kuizidi Prisons kwa pointi nne mpaka sasa.

Coastal imecheza michezo 26, ikishinda mechi 10, sare saba na kupoteza michezo tisa ikibakisha mechi nne kumaliza msimu wa ligi.

Kama iking'ang'ania nafasi hiyo na kumaliza nafasi ya nne hadi mwishoni mwa msimu, Coastal Union inaweza kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika, kama bingwa na Kombe la FA atamaliza kwenye moja kati ya nafasi tatu za juu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu ambayo inaweza kuifanya Coastal kukosa nafasi ya kucheza michuano ya kimataifa mwakani ni Ihefu pekee kama itachukua Kombe la FA, lakini kama litatwaliwa na Yanga au Azam, na yenyewe ikamaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu, basi moja kwa moja itacheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Kanuni ya Bodi ya Ligi inasema kuwa iwapo timu itashika nafasi ya kwanza na pili kwenye Ligi Kuu itacheza Ligi ya Mabingwa Afrika hata kama itatwaa Kombe la FA, huku itakayoshika nafasi ya tatu itacheza Kombe la Shirikisho Afrika kupitia tiketi ya ligi.

Kanuni hiyo inasema timu zilizoshika nafasi tatu za juu kwenye ligi, iwapo zitatwaa ubingwa wa FA, basi timu inayoshika nafasi ya nne itachukua nafasi moja. Timu yoyote ambayo haipo kwenye nafasi hizo za juu, ikitwaa Kombe la FA, inakuwa imejikatia tiketi kucheza Kombe la Shirikisho.

Prisons na KMC ndizo zinazoonekana kuifukuza Coastal kuwania nafasi ya nne zote zikiwa na pointi 33, lakini zikizidiwa pointi nne, huku kila timu ikiwa imebakisha michezo minne.



Wachezaji wa Tabora United wakiwa kwenye mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa leo dhidi ya Mashujaa United kwenye uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora. **PICHA: TABORA UNITED**

## Massawe: Najitunza kulinda kiwango changu

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kuifungia timu yake mabao muhimu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC iliyochezwa juzi, kiungo mshambuliaji wa Mtibwa Sugar, Jacob Massawe, amesema siri ya kuwa na kiwango bora inatokana na kujitunza.

Namungo ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Geita Gold na kufikisha pointi 30, zilizowapaisha hadi katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Massawe, ambaye ni nahodha wa timu hiyo alisema amekuwa mtulivu na anafuata maelekezo kutoka kwa makocha wake, jambo ambalo linamfanya apate namba katika kikosi cha kwanza.

Massawe alisema anaamini ataendelea kuwa mchezaji muhimu katika timu yake na anawataka wachezaji wanaochipukia kujitunza ili kucheza kwa muda mrefu.

"Ili uwe katika kiwango bora ni lazima ujitunze, usikilize vyema maelekezo ya makocha, lakini pia ni lazima uache au upunguze vitu ambavyo vitakupunguzia ubora wako, hii ndio siri yangu kubwa inayofanya niendelee kuaminiwa," alisema Massawe.

Mchezaji huyo alisema anaamini bado ana muda mrefu wa kucheza soka tofauti na baadhi ya mashabiki na wadau wa soka wanavyomwangalia.

" Nina kama miaka mitano mbele ya kucheza mpira kwenye ubora, sina hofu na hilo," nyota huyo wa zamani wa Stand United ya mkoani Shinyanga alisema.

Namungo imeshafika Dodoma kwa ajili ya kujiandaa kuwavaa wenyeji, Dodoma Jiji katika mechi ya raundi ya 27 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Jamhuri.

## Mgunda: Tumefuata pointi tatu Kagera

INATOKA UK. 24

zozitaka," alisema Mgunda.

Aidha, Kocha wa Kagera Sugar, Fred Felix 'Minziro' akizungumzia mchezo wa leo, alisema anafahamu utakuwa mchezo mgumu lakini wamejipanga vyema kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kwenye uwanja wao wa nyumbani.

"Simba ni timu nzuri, ina wachezaji wenye uzoefu, lakini hilo halitutishi, tumejiandaa na naamini tutapata matokeo mazuri tunayoyahitaji.

Endapo Simba itafanikiwa kupata pointi tatu itafikisha idadi ya pointi 57 na kuiondoa Azam yenye pointi 56 kwenye nafasi ya pili katika msimamo wa ligi inayoongozwa na Yanga wenye pointi 68.

## Yanga yaongoza kwa 'clean sheets' Ligi Kuu, kocha Gamondi achekelea

INATOKA UK. 24

kufunga mlango wetu, kucheza bila kuruhusu bao, hii ni muhimu sana katika mpira wa miguu, unatakiwa kwanza kufunga mlango wako, halafu hata kama ukipata bao moja tu una uhakika wa ushindi, kwetu kitu hiki ni muhimu na ndicho kimetuweka sehemu nzuri si kwenye Ligi Kuu tu, bali hata kwenye Kombe la FA," alisema kocha huyo.

Wakati Yanga ikiongoza kwa 'clean sheets' 15 kwenye Ligi Kuu, timu ya Azam FC inafuatia ikiwa haijaruhusu bao katika michezo 13, huku mingine 13 ikiruhusu wavu wake kugushwa katika michezo 26 ambayo imekipiga mpaka sasa.

Kama ambavyo ilivyo kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Yanga ikiongoza, Azam ikifuatia, hata kwenye 'clean sheets' ni hivyo hivyo, Simba ikikamata nafasi ya tatu, yenyewe ikiwa imecheza mechi 11 bila kuruhusu bao, ikicheza michezo 14 ambayo imeruhusu wavu wake kuguswa.



# Michezo

Jumapili Mei 12, 2024

Nipashe





**Mbappe atangaza rasmi kuondoka PSG**

UKURASA 22



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na akimvalisha medali Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ya ushiriki wa mbio za Mbeya Tulia Marathon 2024, zilizoanzia na kuishia kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya jana. **PICHA: OWM**

# MGUNDA: TUMEFUATA POINTI TATU KAGERA

## ●●● Asema morali ya wachezaji ipo juu, Kibu aanza mazoezi mepesi lakini kuukosa mchezo wa leo kama....

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI leo ikiwakabili Kagera Sugar ugenini kwenye uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, kocha wa Simba, Juma Mgunda amesema morali ya wachezaji wake inampa matumaini ya kuondoka na pointi tatu walizozifuata mkoani Kagera.

Simba leo itakuwa mgeni wa Kagera Sugar kwenye mchezo wa ligi kuu Tanzania Bara ikisaka pointi tatu muhimu ili kuendelea kuifukuzia Yanga inayoongoza ligi.

Akizungumza muda mfupi baada ya kufanya mazoezi ya mwisho jana, Mgunda, alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo muhimu na wamechukua tahadhari zote.

"Tahadhari ni muhimu, Kagera ni timu nzuri na inatoa upinzani inapocheza zaidi nyumbani, furaha yangu ni kuona morali ya wachezaji wangu kuwa juu, tumekuja Kagera kwa lengo la kusaka pointi tatu hilo ndio jambo muhimu zaidi," alisema Mgunda.

Alisema katika kikosi chake ataendelea kuwakosa nyota wake, Kibu Dennis na Clatous Chama ambao bado wanaendelea kuuguza majeraha yao.

"Taarifa nzuri Kibu ameanza mazoezi mepesi ingawa ni ngumu kumtumia leo, lakini nina uhakika mchezaji yeyote atakayepata nafasi ya kuanza kesho (leo) ataonyesha uwezo na kuipambania timu," alisema Mgunda.

Alisema amewataka wachezaji wake kusahau ushindi wao kwenye mchezo uliopita dhidi ya Azam na kuweka mkazo kwenye mchezo wa leo ili kuendeleza ushindi.

"Matokeo ya mchezo uliopita yaliishia pale pale uwanjani, kwa sasa lazima tuangalie mbele, muhimu ni kuweka mkazo na mawazo yetu kwenye mchezo wa kesho (leo), kikubwa ni pointi tatu ndizo tuna-

INAENDELEA UK 23

## Yanga yaongoza kwa 'clean sheets' Ligi Kuu, kocha Gamondi achekelea

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Miguel Gamondi ameeleza kufurahishwa na timu yake kucheza mechi nyingi za Ligi Kuu bila kuruhusu bao kitu ambacho amesema ndiyo msingi wa timu inayotaka kuwa bingwa na kutwaa mataji.

Yanga mpaka sasa ndiyo timu inayoongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao ambapo mpaka sasa haijaruhusu wavu wake kuguswa kwenye michezo 15, kati ya mechi 26 ilizocheza kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Imeruhusu mabao katika michezo 11 tu, na katika mechi hizo imeruhusu kufungwa mabao mawili mara tatu tu katika mechi moja, mara mbili dhidi ya Azam, iliposhinda mabao 3-2, Oktoba 23 mwaka jana, na ilipofungwa mabao 2-1 na matajiri hao wa Chamazi Machi 17 mwaka huu.

Pia iliruhusu idadi hiyo ya mabao ilipofungwa na Ihefu, Oktoba 4 mwaka jana.

Pia hajaruhusu bao lolote mpaka sasa tangu ilipofanya hivyo dhidi ya Simba, Aprili 20, iliposhinda mabao 2-1, lakini kuanzia hapo ilicheza mechi nne za Ligi Kuu bila kuruhusu wavu kuguswa na kutoka suluhu dhidi ya JKT Tanzania, ikapata ushindi wa bao 1-0 kwenye michezo dhidi ya Coastal Union, Mashujaa FC na Kagera Sugar bao 1-0..

Akizungumza jijini Dar es Salaam siku chache kabla ya kwenda Morogoro kukipiga dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Gamondi alisema wanachama na mashabiki wa Yanga wanafurahia matokeo mazuri ya ushindi na kukaribia kutwaa ubingwa, lakini yeye anafurahia zaidi timu yake inavyocheza bila kuruhusu bao katika mechi za Ligi Kuu.

"Mimi furaha yangu kubwa ni kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, najua tumecheza mechi nyingi hatukuruhusu bao, lakini kwa siku za karibuni nakumbuka mechi dhidi ya Simba, hatukupata 'clean sheets', ila baada ya hapo tukarudi kwenye hali yetu ya

INAENDELEA UK 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >